epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US

# Nipashe

Jumatatu Mei 13, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581675
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital




# Uchaguzi kanda CHADEMA moto

• **Lissu** asema ni mkakati, wagombea 200 wafanyiwa usaili mkali...*Ukurasa 2*



Baadhi ya wagombea wa nafasi mbalimbali za uongozi wa Kanda Chadema wakisubiri kuhojiwa na Kamati Kuu ya chama hicho kilichofanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: ELIZABETH ZAYA**

UKURASA WA 3

**MHADHIRI UDSM AKERWA UTITIRI TOZO WAWEKEZAJI**

## Wataalamu wataja mbinu za kuepuka hasara ATCL

UKURASA 2

**Kilio** intaneti kusuasua, TCRA yaanika tatizo



UKURASA 19

**Anusurika** kifo madai ya kuiba mtoto, walimu wamwokoa

UKURASA 7



**Makamu** wa Rais ashtushwa wimbi vijana tegemezi

UKURASA 18



RIPOTI YA UCHUNGUZI

## Uwanja wa Benjamin Mkapa haukujengwa kuwa wa kimataifa

UK. 4

**MICHEZO** SIMBA YARUHUSU YANGA KUTANGAZA UBINGWA UK.24

**KATUNI** UK.6




Mafundi wakikata sehemu za barabara iliyoharibika na kuziba upya katika barabara ya Mwai Kibaki Mikocheni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Uchaguzi kanda CHADEMA moto

**Na Elizabeth Zaya**

UCHAGUZI wa kanda za Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) 'ni wa moto', safari hii kuna usaili maalum kwa wagombea katika kanda nne zinazotarajiwa kufanya uchaguzi hivi karibuni.

Jana wagombea wote katika nafasi hizo pamoja na wanaogombea kwenye mabaraza yake kutoka kwenye kanda hizo waliitwa makao makuu ya chama hicho kwa ajili ya usaili na Kamati Kuu ya chama iliyoanza vikao vyake Mei 11, mwaka huu.

Kwa mujibu wa wagombea wa nafasi mbalimbali waliozungumza na Nipashe, hatua hiyo ya kuita wagombea wote na kuwafanyia usaili imechukuliwa kwa mara ya kwanza na wanaamini huenda ni kutaka kufanya uchaguzi wa kimkakati na kupata viongozi ambao watakuwa na uhakika nao kuelekea uchaguzi hizo wa serikali za mitaa na Uchaguzi Mkuu.

Watiania walioitwa kwa ajili ya kufanyiwa usaili kwenye kanda hizo nne ni kwa nafasi za Uenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu na Mhazini pamoja na watiania kwenye mabaraza ya Vijana na Wanawake.

Kwa taarifa ambazo gazeti hili limezipata ni kwamba Kamati Kuu ya CHADEMA, kwa hatua hiyo, itakuwa na uhakika inapopitisha wagombea watakaokuwa wamejitokeza katika nafasi mbalimbali au kukata wengine endapo watabainika kukosa sifa zinazohitajika.

Mgombea wa nafasi ya Uenyekiti Kanda ya Serengeti, Emmanuel Ntobi, alisema uchaguzi wa mwaka huu umekuwa wa tofauti; kwanza mwitikio mkubwa wa watiania katika nafasi mbalimbali tofauti na miaka mingine, pia watiania wote katika kanda nne kufanyiwa usaili na Kamati Kuu makao makuu ya chama.

"Kuna mnyukano mkali uchaguzi huu, lakini sisi tunaamini kwamba chama kinakua, ndio maana hata ushindani unazidi kuwa mkubwa," alisema Ntobi.

Ester Jackson, ni mtiania kwenye afasi ya Makamu Mwenyekiti Kanda ya Serengeti, alisema usaili ulivyokuwa unafanyika kwenye kanda, watiania walikuwa na tabia ya kwenda na wapambe, lakini wanapokusanywa makao makuu hakuna nafasi hiyo.

Mwenyekiti wa CHADEMA Mkoa wa Katavi ambaye ni mtiania Kanda ya Magharibi, Rhoda Kunchela alisema walikuwa wamezoea wanafuatwa kwenye kanda na watu wachache , lakini kwa sasa ni tofauti.

"Miaka ya nyuma ilikuwa inatufuata tena tunafanyiwa na watu sita au saba lakini kwa sasa unakwenda kusimama mbele ya watu zaidi ya 20, hii inaonesha chama kinafanya kazi kwa umakini," alisema Rhoda.

Mwenyekiti Kanda ya Nyasa, Mch. Peter Msigwa anayetia nia kwa mara nyingine kutetea nafasi yake hiyo, alisema katika uchaguzi huo ana uhakika wa kushinda kwa asilimia zaidi ya 80.

"Ni kweli Kanda ya Nyasa ni kwa moto na sababu ya yote hayo ni kwa sababu ya kazi kubwa ambayo nimeifanya na kuifanya ijulikane zaidi kuliko nyingine, na hata safari hii nina uhakika wa kushinda kwa kishindo na sitishwi na mtu yeyote," alitamba Mch. Msigwa.

Makamu Mwenyekiti wa Chama hicho Bara, Tundu Lissu alisema uchaguzi wowote unaofanyika lazima uwe wa mkakati.

"Kwahiyo, hata unavyoniuliza hivyo, ni kweli nikujibu kwamba tunafanya uchaguzi wa kimkakati, uchaguzi siku zote huwa ni mkakati, kujenga chama, kushinda kwenye uchaguzi wa serikali," alisema Lissu.

Alipoulizwa kama kuna uwezekekano wa kuengua baadhi ya wagombea, Lissu alisema iwapo itabidi kufanya hivyo, wataengua kulingana na sifa.

"Kama kawaida ya chama chochote, wagombea wanateuliwa au kutokuteuliwa kama wamekidhi vigezo, hiyo ni kawaida kwa chama. Kwahiyo, uwezekano wa 'huyu anatosha', 'huyu hatoshi' ni kawaida," alisema Lissu.

Mkurugenzj wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa chama hicho, John Mrema alisema baada ya kumalizika kwa uchaguzi huo wa kanda, utafuata wa uongozi wa juu wa chama ukiwamo wa Mwenyekiti wa chama hicho.

Jana Nipashe lilishuhudia wagombea hao wakiwa wamejikusanya katika makundi makundi huku mijadala yao ikitekwa na mshangao wa idadi kubwa ya wagombea waliojitokeza mwaka huu.

Kikao hicho cha Kamati Kuu ya CHADEMA kimeitishwa kukiwa na mjadala unaoendelea kwenye mitandao ya kijamii kuhusu kauli zilizotolewa hivi karibuni na Lissu, hasa ile ya madai ya kuwapo fedha chafu katika uchaguzi wa ndani wa chama hicho.

# Wataalam wataja mbinu za kuepuka hasara ATCL

**Na Jenifer Gilla**

WATAALAM wa uchumi nchini wamewashauri wanasiasa na viongozi wa juu serikalini kuliacha Shirika la Ndege Tanzania (ATCL), lijiendeshe kibiashara bila kuingiliwa.

Aidha, wameishauri serikali kufikiria suala la kushirikiana na sekta binafsi wakati wa utekelezaji wa kuliboresha shirika hilo ili lisiendelee kuleta hasara.

Walitoa kauli hiyo baada ya mjadala wa watu mbalimbali wakiwamo wanasiasa kuitupia lawama serikali kuweka nguvu kwa kuendelea kununua ndege licha ya kujiendesha kwa hasara.

Akizungumza na mwandishi wa gazeti hili, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) mstaafu, Ludovick Utouh alisema ni mapema mno kuanza kuilaumu serikali na kwamba ni muhimu wadau hao wakaipa muda wa angalau miaka mitano kama halitoingiza faida, wana haki ya kuwaadhibu wahusika.

Alisema mchakato wa kulifufua shirika hadi kuanza kuleta faida unachukua muda mrefu na kuwasihi wanasiasa, viongozi wa juu na jamii kuiacha serikali ifanye kazi yake.

Alisema shirika hilo lilikuwa limekufa kabisa ni serikali ya awamu ya tano iliyokuja na msukumo wa kuliamsha na kuwasihi Watanzania wasiwe waoga wa shirika hilo kuleta hasara wakati linafufuliwa.

Kuhusu malalamiko ya serikali kununua ndege, alisema zilizopo hazitoshelezi ndio maana kuna wakati safari zinasitishwa, kwa kuwa ndege inayoelekea eneo fulani ikipata hitilafu hakuna ndege nyingine ya kuwapeleka abiria.

Alitoa mfano wa Shirika la Ndege la Ethiopia ambalo ndio shirika pekee Afrika linalofanya kazi kibiashara na kwa faida, licha ya kuwa na ndege 144 bado wanaendelea kununua nyingine na kuwataka Watanzania suala la kununua ndege lisiwatie hofu.

**USHAURI KWA SERIKALI**

Alitaja moja ya vitu ambavyo serikali inapaswa kujiridhisha kabla ya kuliboresha shirika hilo ni miundombinu ya kutosha ya kufanyia ukarabati ndege hizo zinapopata hitilafu ndogo badala ya kuzirudisha zilipononuliwa.

Aliishauri pia kutafuta maoni ya namna ya kuliendesha shirika hilo ili lilete faida kwa watu mbalimbali akiwamo Mdhibiti Mkuu na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa kuwa peke yake haitoweza.

"Nakumbuka hata mimi nilivyokuwa CAG nilishauri kwamba shirika hili ni muhimu lifufuliwe, ukiangalia sasa hivi uchumi wetu unakuwa kwa kasi baada ya Royal Tour ya Rais Samia Suluhu Hassan, utalii umekuwa sana hivyo usafiri wa anga ni muhimu," alibainisha.

Alitaja eneo lingine la kuliingizia shirika hilo faida ni uwekezaji wa serikali katika kilimo cha parachichi kwa ajili ya kuuza nje ya nchi, kuwa ili soko hilo lifanikiwe linahitaji usafiri wa anga wa uhakika.

Mtaalam wa Uchumi, Prof. Samwel Wangwe aliishauri serikali kujiuliza kuwa linataka kuliinua shirika hilo kwa malengo ya kujiingizia faida au kutoa huduma nzuri kwa ajili ya kuendesha kitu kingine.

Aidha, alishauri pia kufikiria suala la kushirikiana na kampuni nyingine kuendesha biashara hiyo, kwa kuwa yapo mashirika yanayoweza kuendesha shirika hilo na serikali ikapata faida nzuri badala ya kujiendesha yenyewe kwa hasara.

Ripoti ya CAG ya mwaka wa fedha 2022/23 ilionyesha kuwa ATCL imepata hasara ya Sh. bilioni 56.64, sawa na ongezeko la asilimia 62 kutoka hasara ya Sh. bilioni 35.23 iliyoripotiwa mwaka uliopita.

Ilibainisha kuwa sababu za shirika hilo kupata hasara kuwa ni pamoja na kuwapo kwa gharama kubwa za uendeshaji na zisizoepukika kama ukodishaji na bima kwa ndege ya Airbus A220 -300 isiyofanya kazi kutokana na matatizo ya kiufundi kama vile kutu na kasoro za injini.

# Mhadhiri UDSM akerwa utitiri tozo wawekezaji

**Na Joseph Mwendapole**

MHADHIRI wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Shule Kuu ya Biashara (UDBS), Patrolik Kanje, ameshauri utitiri wa tozo za mamlaka ya udhibiti upunguzwe ili kuwapunguzia mzigo wazalishaji wa bidhaa nchini.

Alitoa ushauri huo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na wanachama wa Shirikisho la Wenye Viwanda nchini (CTI).

Alikuwa akiwasilisha matokeo ya utafiti alioufanya kuhusu matatizo ya kisera na ya kikodi yanayozikumba sekta za mazao ya chakula, mazao ya pamba na nguo na kwenye dawa na vifaatiba.

Alisema utafiti huo aliufanya kwenye mikoa mbalimbali kwa kuangalia wenye viwanda na kubaini kuwa gharama za kodi na ada mbalimbali ni kubwa kutokana na mamlaka za usimamizi nyingi kuchukua tozo kwa wazalishaji kwa kitu kile kile.

"Mfano unakuta mchakataji wa maziwa inabidi awe na leseni ya biashara kwenye halmashauri ambayo anafanyia kazi, lakini pia anatakiwa apate leseni kwa msimamizi wa sekta ya maziwa ambayo ni bodi ya maziwa sasa hii inaongeza gharama za uzalishaji kwasababu mtu anaacha kazi zake anafuatilia leseni na anafuatilia kwa huyu na yule," alisema.

"Tunajua kwamba sheria, sera na miongozo mbalimbali inawekwa na serikali ili kuhakikisha mambo yanakwenda vizuri, lakini utekelezaji wake umekuwa na ukakasi kidogo ndiyo maana tunashauri kusiwe na utitiri wa mamlaka za udhibiti kwenye kitu kile kile," alisema.

Alisema licha ya kumpotezea muda mwingi mzalishaji kufanyiwa ukaguzi wa mara kwa mara pia zimekuwa zikiwaongezea gharama kwa kuwa wanapofanya tathimini ya athari kwa mazingira wanalazimika kulipa gharama kwa mamlaka husika au kwa mkandarasi mshauri anayemfanyia kazi.

"Kwa hiyo unakuta ni kitu kile kile ila kinalipwa kwa mamlaka zaidi ya moja kwa mfano kwenye suala la afya kwa wafanyakazi OSHA ndiye anasimamia, akija kwako atakukagua na utalipia cheti, lakini bibi afya wa Manispaa atakuja naye atasema wafanyakazi wapimwe afya na akupe cheti sasa muda wa kupima wafanyakazi unapotea na analipa tena gharama," alisema na kuongeza:

"Hali hii inasababisha gharama za uzalishaji kupanda na bidhaa kushindwa kushindana na zile zinazotoka nje ambazo wakati mwingine zinakuwa nafuu na matokeo yake unakuta viwanda vyetu viunashindwa kushindana vinafungwa," alisema.

Mtaalamu wa Sera ya Viwanda wa Shirikisho la Wenye Viwanda (CTI), Isack Msungu alisema utafiti huo ulifadhiliwa na Shirikisho la Viwanda la Denmark (DI) kuangalia sekta ya pamba, dawa na vifaa tiba na vyakula ambavyo hazijafanya vizuri kama zinavyotakiwa kufanya na nini kifanyike ili kuziwezesha kufanya vizuri.

"Utafiti umeshafanyika na hapa tunawasilisha kwa wadau wetu yaliyotokana na utafiti huo kuangalia namna ya kuishauri serikali na kuishawishi kuchukua haya mapendekezo kwaajili ya utekelezaji ili kuiwezesha sekta hii ifanye vizuri zaidi," alisema.

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BENKI KUU YA TANZANIA

## TAARIFA KWA UMMA

### KATAZO LA KUJIHUSISHA NA BIASHARA YA KUKOPESHA KIDIGITALI BILA LESENI KUTOKA BENKI KUU YA TANZANIA

Benki Kuu ya Tanzania inapenda kuufahamisha Umma kwamba chini ya kifungu cha 17 cha Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha, 2018, Benki Kuu ya Tanzania ina mamlaka pekee ya kutoa leseni kwa taasisi, makampuni, au watu binafsi wanaojihusisha na kutoa mikopo. Pia, kwa mujibu wa kifungu cha 16 (1) cha sheria hiyo, ni kinyume cha sheria kujihusisha na biashara ya kukopesha bila kuwa na leseni. Katazo hili linajumuisha utoaji wa mikopo kwa njia mbalimbali ikiwemo utoaji wa mikopo kwa njia ya Kidigitali bila kuwa na leseni.

Aidha, Benki Kuu inaukumbusha Umma kusoma kwa makini na kuelewa makubaliano wanayoingia na wakopeshaji, ikiwa ni pamoja na kuelewa masharti ya mkopo, na kuhakikisha kwamba mkopeshaji ana leseni halali ya kufanya biashara ya kukopesha. Mkopaji anapaswa kupewa nakala ya mkataba uliosainiwa kwa njia sahihi, na nakala hiyo inapaswa kutolewa kila mkopeshaji anapotoa mkopo mpya.

Benki Kuu inaendelea kuusisitiza Umma kujiepusha kufanya biashara na taasisi, makampuni, au watu binafsi wanaotoa huduma za kukopesha bila kuwa na leseni halali iliyotolewa na Benki Kuu. Aidha, Umma unaombwa kutoa taarifa Benki Kuu na vyombo vya usalama juu ya taasisi, makampuni au watu binafsi wanaofanya biashara bila kuwa na leseni au kutozingatia taratibu zilizowekwa kwa ajili ya kuchukuwa hatua za kisheria. Benki Kuu imetoa orodha ya taasisi, makampuni, na watu binafsi walio na leseni za biashara za kukopesha kwenye tovuti yake: www.bot.go.tz.

Kwa taarifa zaidi tafadhali wasiliana na:- Kurugenzi ya Usimamizi wa Sekta ya Fedha, Idara ya Usimamizi wa Taasisi za Huduma Ndogo za Fedha, Benki Kuu ya Tanzania, 2 Mtaa wa Mirambo, S. L. P 2939, 11884 Dar es Salaam, Simu Na. +255 22 223 5585; Barua Pepe: info@bot.go.tz or botcommunications@bot.go.tz.

**Emmanuel M. Tutuba**
**GAVANA**
**BENKI KUU YA TANZANIA**

16 Barabara ya Jakaya Kikwete, S. L. P. 2303, 40184 Dodoma – Tanzania
Email: governoroffice@bot.go.tz Website: www.bot.go.tz, Simu: +255 22 223 2000/3000/3215/2501
Simu ya Mezani +255 22 223 3021/3022




Vigezo na Masharti Kuzingatiwa

Kwa mawasiliano zaidi Tupigie: 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Barua pepe: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

RIPOTI YA UCHUNGUZI

# Uwanja wa Benjamin Mkapa haukujengwa kuwa wa kimataifa

Na Sanula Athanas

KAMPUNI inayorekebisha Uwanja wa Benjamin Mkapa, jijini Dar es Salaam imethibitisha uwanja huo haukujengwa kuwa wa kimataifa - yaani wa Daraja "A".

Imesema uwanja huo ulijengwa rasmi kuwa wa Daraja la Pili - yaani Daraja "B" ambalo "ndiyo yalikuwa mahitaji ya serikali wakati huo".

Beijing Construction Engineering Group (BCEG), iliyojenga uwanja huo kuanzia mwaka 2004 hadi 2007, ndiyo imepewa zabuni ya kuongeza miundombinu ya uwanja ambayo haikuwekwa awali, kurekebisha na kuhuisha maeneo ambayo ama yameharibika au hayakufikia viwango vya kimataifa. Uwanja ulikabidhiwa rasmi serikalini Julai 3, 2013.

Li Liang, Meneja Mradi wa BCEG, anasema mambo yote hayo yakikamilishwa, uwanja huo utakuwa wa Daraja la Kwanza, yaani Daraja "A" la Shirikisho la Soka Ulimwenguni (FIFA).

Tangu uwanja ulipoanza kutumika miaka 17 iliyopita, kumekuwa na mjadala, watu wakihoji kwanini serikali iliupokea ilhali haukidhi "viwango vya kimataifa".

Kuna waliotaka kujua nani alichora ramani ya uwanja, nani alikuwa msimamizi wa ujenzi, nani hasa alikabidhiwa uwanja huo na kama aliukagua na kuthibitisha kuwa umekamilika kulingana na mchoro wa usanifu wa uwanja uliokamilika.

Hata hivyo, hadhi uliyonayo sasa ya Daraja "B", inakinzana na dhamira ya mwasisi wa mradi huo, Rais wa Awamu ya Tatu, Benjamin Mkapa ambaye mwaka 2000 aliahidi kujenga uwanja wenye hadhi ya kimataifa, yaani Daraja "A", akisisitiza, "ni aibu nchi kukosa uwanja wa kisasa".


Shirikisho la Soka Afrika (CAF), baada ya wataalamu wake kuukagua, limeunga mkono hoja kwamba uwanja huo haukidhi viwango vya kimataifa, hivyo kuelekeza ufanyiwe maboresho.

Kwa mujibu wa Meneja wa Uwanja wa Mkapa, Milinde Mahona, tangu mwanzoni mwa mwaka jana, CAF imekuwa inatuma wataalamu wake kukagua uwanja huo ili utumike katika mashindano yake.

Anataja mashindano hayo ni pamoja na Ligi ya Soka Afrika (AFL), Mataifa ya Afrika (AFCON) 2027 na michuano ya Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) iliyopangwa kufanyika nchini Septemba mwaka huu.

Meneja Mahona anasema timu ya mwisho ya wataalamu wa CAF ilizuru nchini mwishoni mwa mwezi Machi mwaka huu na kukagua uwanja huo kama unafaa kutumika katika mashindano ya CHAN 2024.

Ofisa Usalama wa FIFA nchini, Inspekta Hashim Abdallah na Mkurugenzi wa Habari na Masoko wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Boniface Wambura waliokuwa sehemu ya timu ya ukaguzi wa CAF, kwa nyakati tofauti wametoa ufafanuzi kwa mwandishi wa habari hizi kwamba ripoti ya ukaguzi inadokeza maeneo tofauti yenye upungufu.




Hayo ni pamoja na uwanja huo kukosa; eneo lenye sifa za kuketi waandishi wa habari, alama zinazoongoza waendao majukwaani, miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu na vifaa vya kutambua vyuma (silaha). Pia barabara kupita pembeni mwa uwanja.

Vyote hivi ni miongoni mwa vigezo 89 vya FIFA vinavyotakiwa kukidhi viwango vya viwanja na vilipaswa kuwapo wakati uwanja unakabidhiwa rasmi kwa serikali Julai 3, 2013.

Sasa serikali imesimamisha matumizi ya uwanja huo, isipokuwa panapokuwa na maombi maalum ya mechi za kimataifa na kitaifa, zikijumuisha zinazohusu timu za Azam, Simba na Yanga.

Kutekeleza maelekezo ya CAF, serikali imetoa zabuni ya Sh. bilioni 31 kwa kampuni ileile iliyoujenga, BCEG, ambayo sasa inaendelea na ukarabati kuondoa kasoro zilizoorodheshwa katika ripoti ya CAF kwamba kampuni hiyo ya China haikujenga au haikufikia viwango vya FIFA.

Meneja Mradi wa BCEG, Li Liang, katika ufafanuzi wake kwa mwandishi wa habari hizi, anasema uwanja huo wenye hadhi ya Daraja "B" kwa mujibu wa viwango vya FIFA, unakidhi mahitaji ya ndani ya nchi.

Liang anafafanua kuwa katika madaraja ya viwanja, kuna Daraja "A", "B" na la chini zaidi ambalo ni "C". Anasema lengo la maboresho ya sasa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa ni kukidhi mahitaji ya kimataifa ambayo ni uwanja wa Daraja "A" la FIFA.

Tangu mwaka 2007, uwanja huo wenye uwezo wa kuketisha watazamaji 57,558 umekuwa unatumika kama uwanja wa nyumbani wa timu za Simba na Yanga kwa mechi za ndani na kimataifa, hali kadhalika mechi za nyumbani za Timu ya Taifa ya Soka (Taifa Stars).

Wakati wa utiaji saini mkataba wa maboresho ya uwanja huo Julai 27, 2023, Balozi Dk. Pindi Chana, aliyekuwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, alisema maboresho hayo yanalenga kufikia viwango vinavyotakiwa na FIFA.

"Wito wangu kwa BCEG, hakikisheni kazi hii mnayoifanya iwe ya viwango vilivyowekwa na iendane na ubora na viwango vya CAF na FIFA na ikamilike kwa wakati," Waziri Pindi aliagiza.

Naye aliyekuwa Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Said Yakubu, akafafanua siku hiyo kuwa mkataba huo unaelekeza kufanya maboresho katika vyumba vya wachezaji, chumba cha mikutano ya waandishi wa habari, eneo la watu mashuhuri (VVIP), kubadilisha viti vyote vya watazamaji, kibao cha kuonesha matokeo, kuweka mfumo mpya wa Tehama na kubadilisha kiwanja cha soka (pitch) na seti mbili za magoli.

Pia akataja kubadilisha viti vya benchi la ufundi na wachezaji wa akiba, mifumo ya umeme, taa, majitaka na matangazo uwanjani, eneo la riadha (running tracks), migahawa na kuongeza chumba kwa ajili ya mfumo wa video za kusaidia marefa kutoa uamuzi (VAR).

Katika utekelezaji wake, Yakubu akasema TFF inagharamia viti vipya vitakavyotumiwa na benchi la ufundi na wachezaji wa akiba wakati wa mechi uwanjani na CAF inagharamia maboresho ya kiwanja cha soka kwenye uwanja huo.

**UKAGUZI ULIVYO**

Mkurugenzi wa Habari na Masoko wa TFF, Wambura, anasema ukaguzi wa wataalamu wa CAF umebaini kasoro ambazo ni pamoja na kukosa eneo lenye sifa kwa ajili ya waandishi wa habari na kutokuwa na alama zinazoongoza waendao majukwaani.

Anataja upungufu mwingine waliobaini ni kukosekana miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu, mifumo ya kudhibiti silaha kuingia uwanjani, barabara kupita pembeni mwa uwanja na mashabiki kuingia uwanjani kupitia mageti kwa ajili ya magari.

Akirejea historia ya ujenzi wa uwanja huo ulioanza mwaka 2004, Wambura anasema kuwa mwaka 2006 akiwa Rais wa Chama cha Waandishi wa Habari za Michezo Tanzania (TASWA), waliwasilisha madai ya kuwapo upungufu wa mahali sahihi pa wanahabari kuketi uwanjani, lakini watendaji wa Wizara ya Michezo wakawahakikishia ujenzi wa uwanja umezingatia mahitaji yao.

Hata hivyo, Wambura ambaye aliwahi kuwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB) kwa miaka minne kuanzia Juni 2015 hadi Oktoba 2019, anasema ujenzi ulipokamilika, mahitaji yao ya kuwapo mahali maalum pa kuketi waandishi wa habari hayakuwa yamezingatiwa.

Anafafanua matokeo ya ushuhuda wake kwamba wanahabari walitengewa eneo dogo karibu na jukwaa kuu, chini kushoto mwa jukwaa kuu. Hapo ndipo waandishi kwa miaka mingi wamekuwa wanaketi kwa kujichanganya na

Inaendelea Ukurasa 5




Aliyekuwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Dk. Fenella Mukangara (katikati) akishuhudia aliyekuwa Balozi wa China nchini, Lu Youging akibadilishana hati ya makabidhiano ya Uwanja wa Taifa (sasa Uwanja wa Benjamin Mkapa) na aliyekuwa Kaimu Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Sihaba Nkinga (kulia), jijini Dar es Salaam Julai 3, 2013. **PICHA: MAKTABA**




Eneo jipya la kuketi waandishi wa habari kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa

# Uwanja wa Benjamin Mkapa haukujengwa kuwa wa kimataifa

**Inatoka Ukurasa 4**

mashabiki.

Wambura anabainisha upungufu kwenye eneo hilo kuwa ni kukosekana meza kwa ajili ya wanahabari kuandikia na kuweka vifaa vyao.

Anaonesha kasoro hizo zinavyokinzana na maelekezo ya FIFA, kwamba uwanja wenye hadhi ya kimataifa unapaswa kuwa na eneo kwa ajili ya waandishi wa habari; liwe juu au chini ya jukwaa la VVIP na iwe sehemu katikati inayogawa uwanja pande mbili zinazolingana ili kumwezesha mwandishi wa habari kuona kwa uhakika kinachotokea uwanjani.

Wambura anasema walichokikosoa wao wanahabari mwaka 2006, ndicho kimemulikwa kama kasoro tena wakati ujumbe wa CAF ulipoingia nchini kukagua uwanja huo.

Kwa mujibu wa Wambura, kauli ya CAF ni kuwa "hii si sehemu ya waandishi wa habari; hawawezi kukaa hapo wakichanganyika na mashabiki - hakuna meza za kuandikia, hakuna nafasi ya kutosha".

Ofisa huyo wa TFF mwenye mzizi wa kitaaluma kutoka mwandishi wa habari za michezo, anasema maboresho ya uwanja yanayofanywa hivi sasa, yamezingatia ukosoaji huo wa CAF. Sasa jukwaa la wanahabari limehamishiwa juu ya VVIP ingawa si katikati kama yalivyo maelekezo ya FIFA; liko juu kulia mwa VVIP likiwa na huduma zinazotakiwa.

Mwandishi wa habari hizi alikwenda kuona kinachoendelea uwanjani hapo - Aprili 12 mwaka huu.

Alikuta jukwaa hilo jipya la wanahabari lenye mahitaji yote tajwa, limejengewa njia maalum kuelekea chumba cha mikutano pasi na kuchangamana na watu wengine uwanjani.

Kwenye jukwaa hilo, kuna kibao kwenye meza ya mbele, kinachosomeka kwa lugha ya Kiingereza: 'MEDIA TRIBUNAL'.

Vilevile, mwandishi aliona njia maalum kutoka kwenye jukwaa hilo, ukutani ina maelekezo yanayosomeka kwa lugha ya Kiingereza 'MEDIA CENTRE', ikiambatana na alama za kuonesha kilichoko sehemu tajwa.

Mwandishi alimwuliza mmoja wa wafanyakazi maana ya maneno hayo, naye alijibu, ama kwa ukweli au kwa mzaha, "...sisi tunaona kizunguzungu tu; au kuna kitu wanatuficha".

Kutahitajika tafsiri rasmi ya maneno hayo na mengine kwa Kiswahili ili watumiaji wa uwanja waweze kuelewa kinachotakiwa, kinachokatazwa au kinachoelekezwa.

Ofisa Usalama wa FIFA nchini, Inspekta Abdallah, anasema maboresho ya jukwaa la wanahabari yalifanywa Oktoba mwaka jana kwa maelekezo ya CAF ili uwanja utumike katika mashindano mapya ya Ligi ya Soka Afrika (AFL).

Anasema kuwa licha ya Uwanja wa Benjamin Mkapa kutofikia viwango vya kimataifa, wamekuwa wanatoa rukhsa mechi za kimataifa kuchezwa kwenye uwanja huo kwa kuwa hakuna uwanja mbadala nchini.

Mwandishi wa Habari za Michezo wa Gazeti UHURU, Elizabeth John, anajitambulisha ni miongoni mwa waliokumbwa na adha ya jukwaa la zamani la wanahabari, akisema kuwa huko walivunjiwa simu, kompyuta mpakato na kamera na mashabiki "pale mzuka wa mchezo ulipopanda".

Elizabeth anasimulia, "likifungwa goli, huku wewe (mwandishi) unaandika, shabiki anasimama kushangilia goli, unashangaa simu yako tayari ilishafika chini, ishapasuka.

"Mashabiki wanaposhangilia goli wanainuka ghafla, wanagonga simu inadondoka; wengine wanagonga laptop (kompyuta mpakato) na kamera - vinavunjika! Lile eneo pia lilikuwa na kero ya kelele."

Li Liang, Meneja Mradi wa BCEG, anafafanua kuwa katika utekelezaji mkataba wa ukarabati wa uwanja kati yao na serikali, watafanya maboresho zaidi kwenye jukwaa hilo jipya la waandishi wa habari ili kukidhi matakwa ya CAF na FIFA.

Wambura anataja dosari zingine zilizobainishwa Uwanja wa Benjamin Mkapa kuwa ni za kiutawala, akifafanua, "mtu anaweza akawa amekata tiketi ya jukwaa la mzunguko lakini unamkuta yupo geti la kuingia VIP, pale ndipo wanamrudisha kuwa 'wewe wa eneo la mzunguko, huingii huku'.

"Inawezekana watendaji wa serikali waliokuwa wanasimamia ujenzi wa uwanja hawakuwa na sauti au hawakuwa na uelewa wa masuala ya ujenzi wa uwanja na masharti ya FIFA," anaeleza.

Wambura anataja dosari nyingine ambayo imebainika ni uwanja kutokuwa na miundombinu rafiki kwa ajili ya watu wenye ulemavu.

Anasema suala hilo limepewa uzito na wakaguzi wa CAF ambao wameelekeza maboresho ya uwanja yazingatie kundi hilo kwa kuhakikisha njia, vyoo na majukwaa yanakuwa na miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu na pawe na eneo kwa ajili ya kuegesha baiskeli zao (vitimwendo) wanapoingia uwanjani kuangalia mpira.

"Suala la ukaguzi wa silaha nalo ni changamoto kwa sababu, hata vile vifaa vya utambuzi wa chuma kwenye Uwanja wa Mkapa vipo eneo la kuingia VIP tu, na uwanja wetu sasa hivi hata wakaguzi wa CAF na FIFA wameukosoa kwenye ugawaji majukwaa; kwa sababu wakiuangalia wanaona hapa ni VIP A, hapo VIP B, pale VIP C; lakini kwenye uwanja hakupaswi kuwa na VIP nyingi namna hiyo.

Sehemu ulikojengwa uwanja "nayo ni shida nyingine, anaeleza Wambura. Kwa viwanja vya kisasa barabara zote zinaingia uwanjani, lakini sisi uwanja wetu umejengwa kwenye njia. Kuna Taifa Road (Barabara ya Taifa), si unaijua bwana!

Matumizi makubwa ya barabara ile si kuingia Uwanja wa Taifa (Benjamin Mkapa), ni barabara kabisa watu wanapita kwenda wanakojua wenyewe, lakini viwanja vya kisasa barabara zote zinakwenda uwanjani; barabara haipaswi kupita pembeni mwa uwanja, hapana!"

Wambura anasema, hiyo ndiyo sababu "taratibu za FIFA na CAF kutoruhusu tiketi kuuzwa uwanjani - maana yake ndio hiyo. Watu wanunulie mbali huko, wawe wanakuja na kuingia uwanjani bila kusababisha msongamano. Sasa shida ya kwetu sisi, ukiwa na mechi kubwa pale uwanjani, lazima uifunge Barabara ya Taifa.

"Wanapokagua viwanja, wakaguzi wanataka waone njia za watu kuingia na kutoka uwanjani; yaani usiseme tu unakagua uwanja, uangalie watu wanaingiaje, kwa maana ya barabara," Wambura anafafanua.

Kuhusu eneo la kuhifadhi zana za ulinzi, Ofisa Usalama wa FIFA nchini, Inspekta Abdallah, anasema kuwa awali askari wa Jeshi la Polisi na vikosi vingine vya ulinzi na usalama walikuwa wanaingia uwanjani wakiwa na silaha zao, jambo ambalo ni kinyume cha maelekezo ya FIFA.

Anafafanua kuwa ukiukwaji huo wa miongozo ya FIFA ulitokana na uwanja kutokuwa na eneo la kuhifadhi zana za kiulinzi, lakini sasa changamoto hiyo inatatuliwa.

Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa anasema kuwa hadi Aprili 11, mwaka huu, uboreshaji uwanja huo ulikuwa umefikia asilimia 25.

"Tayari tumeshabadili mfumo wa matangazo uwanjani kuwa wa kidigiti na kuboresha vyumba vya wachezaji kubadilishia nguo ambavyo sakafu yake pia imebadilishwa. Tunafumua pia kiwanja cha mpira wa miguu na lile eneo la riadha linabadilishwa ili kuongeza upana.

"Kwa ufupi, tunabadilisha mifumo yote ya maji, umeme, viyoyozi na viti pamoja na kupiga rangi mageti ya uwanja," anasema Msigwa ambaye wakati mkataba wa ukarabati unatiwa saini Julai 27, mwaka jana, alikuwa Mkurugenzi wa Idara ya Habari (MAELEZO) na Msemaji Mkuu wa Serikali.

Mwandishi alipohitaji kujua hatua zilizochukuliwa dhidi ya watendaji wa serikali baada ya ukaguzi kuthitibisha uwanja una dosari, Msigwa alisisitiza kuwa unakidhi viwango vya FIFA na ndiyo maana unatumika kwa mechi za kimataifa, ikiwamo michuano ya CAF ya Klabu Bingwa Afrika.

"Zile dosari wanazosema wakaguzi wa CAF ni zile ambazo wameziona. Walikuja tena nchini wiki tatu zilizopita, kuna baadhi ya vitu (dosari) walviona, na hata ripoti yao ukiisoma, wanasema ukarabati unaendelea," Msigwa anasema.

Hata hivyo, kwa hoja ya Msigwa kwamba uwanja unatumika kwa mechi za kimataifa, Ofisa Usalama wa FIFA nchini, Inspekta Abdallah, kama alivyonukuliwa awali, anasema wanalazimika kutoa rukhsa uwanja huo utumike kwa mashindano ya kimataifa kwa kuwa hakuna uwanja mbadala nchini - yaani uwanja wenye hadhi ya Daraja "A" la FIFA.

Kifungu cha 29 cha Kanuni za Usalama za FIFA kinaelekeza, "Iwapo uwanja haukidhi mahitaji ya kimuundo, kiufundi na kiutendaji yaliyoanishwa katika kanuni hizi na kunatarajiwa kutokea matatizo makubwa ya kiusalama kutokana na upungufu huo, uwanja huo unaweza kuzuiwa kutumika katika mechi za mashindano ya FIFA."

Kwa mujibu wa Meneja Mradi wa BCEG, Li Liang, Uwanja wa Benjamin Mkapa una milango mikubwa mitano, kamera za usalama (CCTV) 114, taa 260 na eneo la kuegesha magari madogo 600 kwa wakati mmoja. Kiwanja chake cha soka kina urefu wa mita 105 na upana wa mita 68.

***FUATILIA KESHO BODI YA USAJILI WA WAHANDISI (ERB) NA BODI YA USAJILI WA MAKANDARASI (CRB) WAKIFICHUA KILICHOSABABISHA KUJENGWA UWANJA WA DARAJA "B" BADALA YA "A"**



Viti vipya kwa ajili ya benchi la ufundi na wachezaji wa akiba

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Makocha kuwa na jazba kwa marefa zaidi ya wachezaji ni hatari

**BAADA** ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya Yanga na Kagera Sugar Jumatano iliyopita, Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam lilitokea tukio la kushangaza pale Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, alipoingia uwanjani akitaka kumkunja mwamuzi wa pembeni wa mchezo huo.

Kocha huyo alitaka kufanya hivyo, kwa kile kilichoelezwa ni kukataa bao lililofungwa na Joseph Guede, ambalo tafsiri ya waamuzi ni kwamba, kabla ya kufunga alikuwa ameotea.

Picha za video zilionekana kocha huyo akiingia uwanjani kuwafuata waamuzi na kutaka kupiga mmoja wa marefa, ambapo kama si juhudi kubwa za wachezaji wa Yanga kumshika na kumsihi na wengine kumng'ang'ania kocha wao asifanye alichokusudia, saa hizi tungekuwa tunasema mengine.

Hatutaki kuingia kwa undani sana kuhusu hilo, lakini kinachoshangaza ni kwamba mechi ilikuwa imeisha kwa Yanga kushinda bao 1-0, hivyo hasira za Gamondi hazijulikani zilitokana na nini. Tunaona hata kama mwamuzi amekosea, lakini kama timu imeshinda, angalau makocha wanatulia na kujidhibiti kwa utovu wowote wa nidhamu.

Tungemuelewa kama timu ingekuwa imepoteza au imetoka sare, ingawa hata hivyo hicho si kigezo cha kocha yeyote kufanya utovu wa nidhamu kwani mara zote tunaamini wachezaji ndio hupatwa na hasira zaidi kutokana na damu zao kuchemka kwa kasi ya mpira.

Tunaamini, Gamondi ambaye ni kocha bora kwa miezi miwili mfululizo na timu yake imekuwa ikifanya vema, huku ikikaribia kutwaa ubingwa, hakupaswa kufanya vile alivyofanya.

Tunajua madhaifu ya waamuzi wa Tanzania, lakini ukweli usemwe tu hakuna timu yoyote hapa nchini, ikiwamo Yanga yenyewe ambayo haijawahi kunufaika na maamuzi yasiyo sahihi ya marefa.

Kama kila kocha akitaka kuchukua sheria mkononi baada ya 'kunyongwa' na maamuzi ya baadhi ya waamuzi kwenye Ligi Kuu, basi ingekuwa ni vurugu tupu.

Tunakumbuka katika mechi ya mzunguko wa kwanza dhidi ya Kagera Sugar iliyochezwa, Februari 2, mwaka jana, Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera, mwamuzi wa pembeni alikataa bao la Kagera Sugar ambalo kwa mujibu wa marudio ya televisheni halikuonekana kuwa na utata wowote, lakini hatukumuona Kocha Fred Felix Minziro alitaka kunyaka kama alivyotaka kukifanya Gamondi.

Sisi tunataka kuona makocha wakiongoza kwa nidhamu na wao wakiwa sehemu ya kuwazuia wachezaji ambao mara nyingi wakiwa mchezoni damu inakuwa imechemka na ni rahisi kwao kufanya matukio kama hayo na si kocha kuonyesha utovu wa nidhamu wa aina hiyo.


Kocha kufanya matukio ya utovu wa nidhamu kama huo, kunaweza kusababisha mashabiki nao kuingia uwanjani na kuhatarisha usalama zaidi, jambo ambalo linaweza kuleta madhara makubwa na si hilo tu bali pia litaishusha ligi yetu ambayo inazidi kukua kila uchao.

Ifike wakati pia makocha waipe thamani na heshima ligi yetu kama ambavyo wanaipa michuano ya kimataifa, kwani kama aliweza kujizuia kuingia uwanjani kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Mamelodi Sundowns pale bao la Stepahe Aziz Ki lilipokataliwa, iweje hii ya Ligi Kuu?.

Kwetu sisi tunamini bao hilo lilikuwa ni muhimu zaidi kwa sababu lingeivusha Yanga hatua ya nusu fainali, na mechi iliisha kwa sare kiasi cha kupigiana mikwaju ya penalti, lakini hili dhidi ya Kagera Sugar tena tayari wameshinda, ni kuikosea heshima ligi yetu.

Hili tunaliachia Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF) na Bodi ya Ligi (TPLB), kuchukua hatua zaidi ili kuzuia vitendo vya kihuni vinavyoweza kuleta madhara makubwa viwanjani.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Timu ziache kusajili kwa mazoea, Ligi Kuu inahitaji wachezaji vijana

**KABLA** hata Ligi Kuu Tanzania Bara haijamalizika, klabu zimeanza mchakato wa kuviimarisha vikosi vyao kwa msimu ujao wa mashindano mbalimbali.

Tumeanza kusikia klabu zikiwa katika harakati za kubakisha wachezaji wao muhimu kwa kuwaongezea mikataba, kuachana na wale wanaoonekana hawakukidhi matarajio, walioshuka viwango na kumaliza mikataba huku wakiwa hawana nia ya kuwaongeza tena.

Vile vile, viongozi wa klabu kwa sasa wanaumiza vichwa kusajili wachezaji wapya wa ndani na nje ya nchi ili kutoa ushindani mkubwa zaidi msimu ujao kuliko huu.

Kila klabu ina malengo yake, kwani kuna zinazosajili wachezaji ili waje kupambania mataji hasa Ligi Kuu Tanzania Bara, Kombe la FA, Kombe la Shirikisho na Ligi ya Mabingwa Afrika, wapo wanaosajili ili waje kupambana kumaliza nne bora kwenye ligi, na wapo viongozi wa klabu japo hawasemi, lakini lengo ni kutaka timu zao zipigane tu kwa ajili ya kusalia Ligi Kuu miaka nenda rudi.

Klabu hizo hazina mpango wa kutwaa ubingwa wala kucheza makombe ya kimataifa, wao wanataka tu pointi za kuwafanya kusalia Ligi Kuu, kwa sababu hata wakipata nafasi za juu, inakuwa mtihani mkubwa kutokana na kutoweza kumudu gharama za maandalizi na usafiri.

Pamoja na hayo, klabu zote hizo zinahitaji usajili, tena wa wachezaji bora. Hata timu zinazotaka kubaki Ligi Kuu zinahitaji wachezaji wazuri ili ziweze kuwapiga bei kwenye klabu kubwa baadaye.

Nitoe ushauri kwa viongozi wa klabu hasa za kati ambazo nimezilenga katika makala hii, kuacha kusajili wachezaji waliocheza kwa muda mrefu Ligi Kuu, badala yake sasa zianze kusaka wachezaji vijana, ambao wameonekana wana uwezo mkubwa kwenye Ligi za Championship, Ligi Daraja la Pili, ('First League'), na pi kwenye mashindani ya vijana chini ya miaka 20 na 17.

Niseme tu kuwa moja ya sababu kubwa ya baadhi ya klabu za kati kutofanya vema kwenye Ligi Kuu ni sababu ya kuwakumbatia wachezaji wale wale, waliocheza Ligi Kuu kwa muda mrefu na wamekuwa wakizunguka kwenye klabu hizi hizi.

Wachezaji hawa wameonekana kabisa hawana jipya au la zaidi watakaloendelea kulitoa kwa sababu wameshafika mwisho wa uwezo wao na umri pia umewatupa mkono.

Kwenye ligi hii kuna wachezaji misimu saba mpaka 10 wanazunguka kwenye timu hizo hizo, na unakuta wameshazichezea timu zote, zikiwamo Simba, Yanga na Azam, lakini pia wapo ambao hawajapitia timu hizo, lakini wameshakipiga na timu zote za kati za Ligi Kuu.

Mchezaji anakuwa ameshachezea Mtibwa Sugar, Polisi Tanzania, Ruvu Shooting, Ihefu, Mashujaa FC, Geita Gold, Dodoma Jiji, Singida Fountain Gate, Kagera Sugar, JKT Tanzania, Namungo, yaani mpaka anawachanganya mashabiki kwani kila msimu ana timu mpya.

Kwa misimu hii miwili ama mitatu, wachezaji hawa hawajaleta tija yoyote, badala yake wamezifanya mpaka timu za Simba, Yanga na Azam ziwe na wigo mdogo wa kusajili wachezaji wa Kitanzania.

Timu hizi haziwezi kuchukua aina hiyo ya wachezaji ambao miaka nenda rudi wapo Ligi Kuu, na wengine wameshawahi kuzichezea klabu zao misimu mitano hadi saba nyuma.

Nitoe ushauri kwa viongozi wa klabu hasa hizi zinazoitwa au kujiita ndogo, zikasajili wachezaji vijana kutoka Ligi ya Championship ambao hawana majina na wameifanya ligi hiyo kuvutia wengi, kiasi kwamba hata dirisha dogo mchezaji kama Emmanuel Mtumbuka wa Stand United, alisajiliwa na Mashujaa FC na anafanya vizuri.

Kule 'First League' kuna wachezaji wazuri tu, na Ligi ya Vijana wapo wachezaji ambao wana uwezo kabisa wa kucheza Ligi Kuu.

Kwanza hawatotumia gharama kubwa za usajili, lakini zitapata wachezaji vijana wanaotafuta majina na kujituma, tatu watakuja kuwauza baadaye.

Tunataka ligi ya msimu ujao iwe na wachezaji wengi wapya vijana kwa manufaa pia ya Timu ya Taifa, Taifa Stars, siyo kila msimu wachezaji ni hao hao wanazunguka kila timu.

# Anusurika kifo madai kutaka kuiba mtoto wa mwaka mmoja

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKAZI Mtaa wa Muhimbili, Halmashauri ya Manispaa ya Lindi, Saidi Mapanga (27), amenusurika kifo baada ya wananchi wenye hasira kumpiga kwa madai ya kuiba mtoto wa mwaka mmoja kwa kile kilichodaiwa imani za ushirikina.

Tukio hilo lilitokea mwishoni mwa wiki karibu na eneo la Shule ya Sekondari Angaza, Halmashauri ya Manispaa hiyo saa saba mchana.

Hafisa Juma anayejihusisha na kazi ya kukaanga mihogo kwenye eneo, alidai kuwa wakati akiendela na shughuli zake, alimwona mtuhumiwa akimshika na kumlambisha mtoto kitu mdomoni kisha kumbeba kuelekea porini, hali iliyomshtua na kuanza kumfuatilia.

Alisema kuwa baada ya kumfuatilia na kumshika shati, alimwuliza mahali anakokuwa anampeleka mtoto huyo, ndipo alimshusha chini na kutaka kukimbia, naye alipiga kelele kuomba msaada kwa wananchi waliojitokeza.

"Mtoto huyu ni wa jirani yangu, tunakaa mtaa mmoja na alikuwa anacheza nje ya nyumba yao, alipofika huyu Bwana akamchukua huku akimlisha kitu kisichojulikana halafu akaondoka naye," alidai.

Hafisa alisimulia kuwa wakati wananchi hao wakiendelea kumpiga, kulijitokeza kundi la walimu kutoka Shule ya Sekondari Angaza ambao walimwokoa mtuhumiwa na kumpa hifadhi katika chumba cha darasa na kuita askari polisi kumchukua.

Baadhi ya walimu wa shule hilo walisema walimwokoa kijana asiuawe. Baada ya kumhoji, alidai alitumwa na mganga kutafuta viungo vya mtoto wa kike.

"Tulipomhoji mtuhumiwa, alidai ametumwa na mganga wa kienyeji amtafutie viungo vya mtoto wa kike mwenye umri usiozidi mwaka mmoja," alidai mmoja wa walimu hao.

Mama mzazi wa mtoto huyo, Halima Yusufu, akizungumzia tukio hilo alisema kuwa siku ya tukio, akiwa anandaa chakula, mwanawe alikuwa anacheza na kaka yake nje ya nyumba yao, lakini kaka yake aliondoka na watoto wengine na kumwacha mdogo wake akicheza peke yake.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, ACP John Imori alipoulizwa kuhusu tukio hilo, alithibitisha kumshikilia mtuhumiwa Mapanga kwa ajili ya mahojiano.

Alisema kuwa watamfikisha mahakamani kujibu shtaka linalomkabili baada kukamilisha upelelezi.

Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (CPA) inaelekeza kuwa baada ya kukamata mtuhumiwa, polisi wanapaswa ama kumfikisha mahakamani ndani ya saa 24 au kumwachia huru, isipokuwa kwa makosa ambayo yanahusiana na adhabu ya kifo.

# Mahakama yaagiza mkurugenzi afike kortini kujieleza asifungwe

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam imemwamuru Mkurugenzi wa Bodi ya Bima ya Amana (DIB), Isack Kihwili, kufika mahakamani Mei 27, 2024 kueleza hali ya utekelezaji hukumu ya mahakama kuhusu malipo ya Sh. bilioni 145.9 kwa Kampuni ya Coast Textile Limited.

Kumbukumbu zinaonesha kuwa Kihwili hajahudhuria mahakamani mara tatu mfululizo kama ilivyoagizwa na mahakama. Alitakiwa kufikia mahakamani Machi 6, 2024, Aprili 18, 2024 na Ijumaa iliyopita (Mei 10, 2024).

Amri hiyo ilitolewa mwishoni wa wiki na Jaji Salma Maghimbi wakati shauri la utekelezaji hukumu iliyotolewa na mahakama takriban miaka tisa iliyopita lilipokuja kwa ajili ya kutajwa.

Mkurugenzi Kihwili siku hiyo alitakiwa kufika mahakamani na kueleza sababu za kutotekeleza hukumu ya mahakama ya mwaka 2015, lakini hakuhudhuria.

Wakili wa Serikali Francis Wilson, ambaye alifika kwa niaba ya Mkurugenzi wa DIB, alifahamisha mahakama kwamba siku ya hiyo, Kihwili alikuwapo asubuhi, lakini aliondoka baadaye kwa kuwa alikuwa na ratiba nyingine ya kuonana na daktari wake.

Kuhusu hali ya malipo hayo, alidai kuwa mfilisi ameanza kuwalipa wenye amana kwanza kulingana na sheria inavyotaka na wadai wengine, kama Coast Textile Limited, watalipwa baadaye. Hata hivyo, Wakili Joseph Rutabingwa, anayeiwakilisha kampuni ya Coast Textile Limited, alipinga hoja hiyo ya Wakili wa Serikali Wilson.

Kuhusu kuhudhuria kwa Kihwil, wakili huyo alida alifika asubuhi katika majengo ya mahakama na hakumwona Mkurugenzi huyo wa DIB.

"Si vyema mtu kuja hapa na kuidanganya mahakama. Ninamfahamu Kihwili. Nimekuwa hapa tangu asubuhi, sikumwona. Ni bora kuiambia mahakama ukweli, hii si mara ya kwanza anapuuza maagizo ya mahakama kuhusu suala hili," alidai

Kuhusu utekelezaji malipo hayo, Wakili Rutabingwa alidai kuwa sheria iko wazi kuwa mtu ambaye ana hukumu ya mahakama mkononi, kama mteja wake, ndiye anayetakiwa kulipwa kwanza na si vinginevyo.

Jaji Maghimbi alimkumbusha Wakili wa Serikali kuwa amri inayomtaka Kihwili kufika mahakama kujieleza kwanini asipelekwe jela kwa kushindwa kutekeleza hukumu ya mahakama bado haijafutwa. Hivyo, akamtaka kufika mahakamani Mei 27, 2024.

Katika vikao vya mahakama vilivyopita, Jaji mwingine aliyekuwa anasikiliza mwenendo wa shauri hilo, Amir Mruma alimwagiza Kihwili kutii notisi iliyomtaka yeye binafsi na si mwakilishi kufika mahakamani na kutoa sababu za kwanini hajatekeleza hukumu hiyo.

Jaji huyo alidokeza kuwa fedha hizo ambazo ndizo zilitolewa katika hukumu hiyo si za serikali, bali ni mali ya Benki ya FBME iliyochukuliwa na Benki Kuu ya Tanzania baada ya kufilisika.

Mei 20, 2022, Jaji Mruma aliamuru Mkurugenzi wa DIB, ambaye aliteuliwa na BoT kuwa mfilisi wa FBME, kulipa kiasi hicho baada ya kukubali maombi ya utekelezaji humumu yaliyowasilishwa na Coast Textiles Limited.

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**NEXT RECOVERY TANZANIA LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS COMPANY LIMITED na MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LTD** kwa idhini tuliyopewa na Benki ya **INTERNATIONAL COMMERCIAL BANK (T) LTD,** tutauza kwa minada ya hadhara nyumba/dhamana zifuatazo baada ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe/siku ya tangazo hili. Nyumba/Viwanja hivi vimewekwa rehani kudhamini mikopo iliyotolewa na benki ya ICBTL kwa wakopaji wafuatao.

**Pia, Tangazo hili la minada ya hadhara,** ni notisi ya siku kumi na nne(14) kwa wakopaji /wadhamini wa mikopo hii kuhusu mauzo ya dhamana zifuatayo kwa minada ya hadhara.

**MCHANGANUO WA DHAMANA ZITAKAZOUZWA**

| NO | JINA LA MKOPAJI/MDHAMINI | TAARIFA ZA DHAMANA | TAREHE YA MNADA | DALALI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | CARGO STAR LIMITED (Mkopaji)<br>LEO JOSEPH MANYARA (Mmiliki/Mdhamini) S.L.P 10000 Dar Es salaam | Nyumba ya makazi yenye hati nambari: 84639, iliyopo kiwanja na. 14 ,kitalu'K', karibu na shule ya msingi ya Mongo la ndege,Ukonga,Manispaa ya Ilala, Dar es Salaam | 03/06/2024 kuanzia saa tatu asubuhi.Mnada utafanyika mahala iliko dhamana tajwa. | NEXT RECOVERY TANZANIA LIMITED Simu:0754262400 |
| 2 | SALVATORY CELESTINE RWABIZI (Mkopaji)<br>HAYDERALI FIDAHUSSEIN KHAKI (Mdhamini/Mmiliki) | Vyumba vya Maduka na Ofisi zilizopo karibu na soko la kisutu kwenye Kiwanja namba. 1374/208 zenye hati nambari zifuatazo<br>i. G2 chumba cha ofisi,Hati namba. 186003/79/1<br>ii. G4 chumba cha ofisi,Hati namba. 186003/79/3<br>Iii.G7 chumba cha duka,Hati namba 186003/79/4<br>Iv.G8 chumba cha duka,Hati namba. 186003/79/5<br>v. G9 chumba cha ofisi,Hati namba. 186003/79/6<br>vi. G10 chumba cha duka,Hati namba.186003/79/7 | 31/05/2024 kuanzia saa tatu asubuhi.Mnada utafanyika mahala iliko dhamana tajwa | NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS COMPANY LIMITED Simu: 0754497396 |
| 3 | SALVATORY CELESTINE RWABIZI (Borrower)<br>SARAH INVESTMENT LIMITED(Mdhamini/Mmiliki) P.O. Box 5829 Dar Es salaam | Nyumba ya vyumba vine ghorofa ya kumi yaani: "Apartment no 10C on 10th floor", iliyojengwa kwenye kiwanja namba 827/22 FLUR II, Hati namba 166900/1/25 Iliyoko maeneo ya 'DTV round about'. | 30/05/2024 kuanzia saa tatu asubuhi. Mnada utafanyika mahala iliko dhamana tajwa | NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS COMPANY LIMITED Simu: 0754497396 |
| 4 | N AND J INVESTMENT LTD (Mkopaji)<br>JOSEPH JAMES MGANA (Mdhamini/Mmiliki) S.L.P 31902 Dar Es salaam | Nyumba yenye hati nambari: 132151, lililopo kiwanja na. 195 ,Kitalu '2', MBWENI MPIJI, KINONDONI – DAR ES SALAAM | 29/05/2024 kuanzia saa kuanzia saa tatu asubuhi.Mnada utafanyika mahala iliko dhamana tajwa | MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LTD Simu: 0755506970 |
| 5 | N AND J INVESTMENT LTD (Mkopaji)<br>JOSEPH JAMES MGANA (Mdhamini/Mmiliki) S.L.P 31902 Dar Es salaam | Nyumba yenye hati nambari: 86341, Kiwanja na. 998, Kawe jirani na Academic International Primary School, Manispaa ya Kinondoni,Dar es Salaam. | 28/05/2024 kuanzia saa kuanzia saa tatu asubuhi.Mnada utafanyika mahala iliko dhamana tajwa | MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LTD Simu: 0755506970 |

Wanunuzi wote wenye nia na uwezo,mnakaribishwa kuja kukagua nyumba/dhamana kwa vigezo na masharti yafuatayo:

**VIGEZO NA MASHARTI YA MNADA;**

1. Mali/Dhamana itauzwa Kama ilivyo.
2. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya nyumba papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14 kutokea siku ya mnada.
3. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa na mnada utarudiwa kwa tarehe nyingine.
4. Gharama za kuhamisha umiliki na kumtoa mdaiwa/mpangaji "Eviction" na nyinginezo, zitakuwa juu ya Mnunuzi.
5. Ukaguzi wa dhamana unaweza kufanywa na wanunuzi, siku yoyote kuanzia siku ya tangazo hili kati ya saa tatu asubuhi na saa kumi na moja jioni.
6. Kwa taarifa zaidi,wasiliana na kampuni husika ya uuzaji .

# Serikali kujenga kituo jumuishi cha parachichi

**Na Mwandishi Wetu,**
RUNGWE

SERIKALI imeanza mchakato wa ujenzi wa kituo jumuishi cha huduma za parachichi ambacho kitasaidia kuhifadhi na kuchakata zao hilo huko Kiwira, Wilaya ya Rungwe, mkoani Mbeya.

Akiwa ziarani mkoani Mbeya mwishoni mwa wiki, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alihoji utatuzi wa changamoto ya kuharibika kwa parachichi katika eneo hilo, Mkurugenzi wa Mazao Wizara ya Kilimo, Enock Nyasebwa alijibu kuwa wako katika hatua za mwisho kukamilisha taratibu za kimkataba ili kumwezesha mkandarasi kuanza ujenzi.

"Ujenzi wa kiwanda hiki utawezesha kuongeza thamani ya zao la parachichi kwani utawezesha wakulima kuhifadhi mazao yao katika chumba baridi pamoja na kuchakata mazao yatokanayo na matunda hayo ikiwamo mafuta," alisema.

Mkurugenzi huyo aliongeza kuwa katika kuongeza zaidi thamani ya zao hilo, wameanza mpqngo wa kuweka vigezo ili kuhakikiwha miche inayopandwa inakiadhi vigezo lengo likiwa ni kupata zao lenye ubora ambayo litafanya vizuri kwenye soko la kimataifa ili kuongeza upatikanaji fedha za kigeni na kukuza uchumi wa mwananchi mmoja mmoja.

Majaliwa alimwagiza mkurugenzi huyo kuhakikisha wanakamilisha taratibu zilizobaki ikiwa ni pamoja na utoaji elimu kwa wananchi kuhusu kilimo bora cha zao la parachichi ili kuongeza thamani na ubora.

Waziri Mkuu alikagua ujenzi wa jengo la utawala la Halmashauri ya Busokelo lililoko eneo la Lwangwa na kuweka jiwe la msingi kwenye jengo hilo.

Awali Mkurugenzi wa Halmashauri ya Busokelo, Loema Peter alimweleza Waziri Mkuu kwamba ujenzi wake umefikia asilimia 94 na akaomba serikali ikamilishe taratibu za upatikanaji Sh. bilioni 2.3 ili wakamilishe hatua iliyobaki.

Alisema hadi hadi sasa wamekwishapokea Sh. bilioni 6.08 za ujenzi na Sh. milioni 300 kwa ajili ya ununuzi wa samani za ofisi hizo.


NMB
Close to you

## REQUEST FOR PROPOSAL FOR SUPPLY OF DUAL INTERFACE EMV CONTACTLESS CARDS

1. NMB Bank Plc is a fully-fledged commercial bank listed at the Dar es Salaam Stock Exchange in Tanzania and has consistently been the most profitable bank in the country over the years. The Bank offers banking services to individuals, small to medium sized businesses, large corporate clients and government. NMB Bank has an extensive physical and digital distribution network, giving its clients choices in accessing banking services.

2. The bank has set aside funds for the **Supply of Dual Interface EMV Contactless Cards.**

3. The bank now invites eligible, qualified, and experienced vendors to participate on the request for Information for the **Supply of Dual Interface EMV Contactless Cards.**

4. The selection and shortlisting of vendors will be conducted through the open competitive tendering as per bank's procurement policy.

5. Interested and eligible vendors shall obtain RFP Instruction document from our website **www.nmbbank.co.tz/tenders** and request for clarifications on the RFP document shall be sent to the office of Secretary, Management Tender Committee at **procurement@nmbbank.co.tz** not later than **Tuesday 21st May 2024**

6. The deadline for submission of the RFP documents will be on **Thursday 30th May 2024 at 15H00 EA Time**. For the hard copy documents, they must be marked on the envelope/email: **Tender for Supply of Dual Interface EMV Contactless Cards.** The RFP Response documents shall be delivered in either of the following ways:-

   - Hard Copy delivery in sealed envelopes and deposited at the TENDER BOX located on ground floor of NMB Bank Head Office, at Ohio/Ali Hassan Mwinyi Road, Dar es salaam; or
   - Delivery by courier and addressed to Secretary, NMB Bank Plc Management Tender Committee P.O. Box 9213, Dar es Salaam; or
   - Email delivery (with password encryption) to - **tendersubmission@nmbbank.co.tz** (maximum document size 20MB)

7. Late tenders, portion of tenders, tenders not received, tenders not opened at the tender opening ceremony shall not be accepted for evaluation irrespective of the circumstances.

**The Chief Executive Officer, NMB Bank Plc**
**NMB Head Office Ohio/Ali Hassan Mwinyi Street**
**P.O. Box 9213, Dar Es Salaam, Tanzania, East Africa**

www.nmbbank.co.tz


## Tanzania, Zambia kuimarisha ufanisi wa huduma za mpakani

**Na Mwandishi Wetu,**
MOMBA

KAMISHNA Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Alphayo Kidata na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Zambia (ZRA), Dingani Banda wameweka mikakati ya kuimarisha utendaji kazi wa mpaka wa Tanzania na Zambia, Tunduma ili kuhudumia kwa ufanisi wasafiri na wasafirishaji kutoka pande zote.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kamishna Kidata alisema wamejipanga kuimarisha mpaka wa kuingia Tanzania na kwenda Zambia.

Alisema wataalamu kutoka Tanzania na Zambia wako imara katika utendaji katika kazi zao za kila siku kwa wafanyabiashara na jamii kwa ujumla.

"Tumekubaliana kwa pamoja kuimarisha utendaji kazi wa mpaka huu kwa sababu ni muhimu kwa maslahi ya nchi zetu na tunaimarisha mifumo ya forodha, ufanisi na uwajibikaji katika kurahisisha mifumo ya uvushaji mizigo na bidhaa na kuzuia mianya yote ya magendo," alisema Kidata.

Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Zambia (ZRA), Dingani Banda, alipopongeza ujio wa Kamishna Mkuu wa TRA, Kidata, ambaye aliongozana na timu ya viongozi mbalimbali kutoka TRA na kuahidi kuwa yeye na timu yake watayafanyia kazi maazimio mbalimbali waliyokubaliana katika mkutano huo na kupanga tena siku nyingine ya kukutana na kupeana mrejesho.

Makamishna hao walijadili na kukubaliana kuimarisha mikakati ya pamoja ya kuboresha mpaka wa Kasesya ulioko wilayani Kalambo, mkoani Rukwa ambao utapunguza msongamano wa magari katika mpaka wa Tunduma.

"Tumekubaliana kuimarisha mpaka wa Kasesya ambao kwetu ni wa kimkakati na nimepita jana (juzi) kujionea mwenyewe hali ilivyo pale kwa sababu ni fursa kwetu," aliongeza Kidata.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka kwa Ofisa Mfawidhi wa Forodha wa TRA, Kassim Mhando, makusanyo ya kodi mpakani huko katika kipindi cha miezi 10, yaani kuanzia mwezi wa Julai, 2023 hadi Aprili, 2024, TRA ilifanikiwa kukusanya jumla ya Sh. bilioni 122.3 kati ya lengo la kukusanya Sh. bilioni 120.5 sawa na ufanisi wa asilimia 101.5.

Alibainisha kuwa mpaka wa Tunduma una wastani wa uvushaji zaidi ya magari 1,000 kwa siku yanayotoka na kuingia Tanzania kutokana na matumizi thabiti ya skana mpya ya kisasa inayoweza kuvusha magari mengi kwa muda mfupi na kuepusha foleni.

"Moja ya faida zinazopatikana katika mpaka huu ni idadi ya mizigo inayokwenda nje ya nchi, inaongezeka mwaka hadi mwaka hali ambayo inapelekea mapato kuongezeka," alisema Mhando.

Alisema hali ya udhibiti wa magendo mpakani kupitia Idara ya Forodha katika Kitengo cha Udhibiti na Ushurutishaji imekuwa nzuri kutokana na kitengo hicho kufanya doria mbalimbali na kimekuwa kinakamata magendo.

Alisema kuwa mwaka huu wa fedha kimekamata jumla ya tani 160 za vipodozi ambavyo vimethibitishwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kuwa havifai kwa matumizi ya binadamu.

Makamishna wote wawili wamekubaliana kwa pamoja kukutana tena mapema mwezi Agosti mwaka huu kwa ajili ya mrejesho wa mambo waliyokubaliana katika kikao walichofanya mjini Tunduma.



# Kaya 34 ‘zagoma’ kuondoka Uwanja wa Ndege K’njaro

**Na Mary Mosha,** HAI

SERIKALI imesema kuna kaya 34 ndani ya eneo la Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), hazijahama licha ya kutakiwa kufanya hivyo.

Kutokana na wananchi hao kutoondoka, serikali imewapa siku saba zaidi waondoke kwa hiari badala ya kusubiri matumizi ya nguvu.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, serikali ilitoa zaidi ya Sh. bilioni 11 kwa ajili ya kuwalipa fidia wananchi waliovamia eneo la Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), sawa na kaya 1,700.

Babu, alifafanua kuwa kila mwananchi mwenye malalamiko ya msingi, wakiwamo wale ambao hawajapata fedha zao kutokana na sababu za mirathi, kukosewa kwa majina na waliokwenda mahakamani, wao hawajavunjiwa nyumba zao wakisubiri maelekezo mengine.

“Sisi tuna watoto, ni wazazi na ni binadamu, hatuwezi kumuonea mtu. Mtu kama hajapata fidia, hakuna mtu anayemvunjia nyumba yake. Wananchi hawa 34 likiwemo kanisa halijavunjwa hadi leo, ila jana wamewekewa fedha,” alisema Babu

Mkuu wa Wilaya ya Hai, Amir Mkalipa, alisema ziko nyumba kadhaa ambazo hazikulipwa fidia kutokana na sababu mbalimbali, lakini tayari serikali na wananchi hao wamekutana na kurekebisha makosa na sasa wameingiziwa fedha zao za fidia Mei 10 mwaka huu.

Mkalipa, alisema asilimia 95 ya wananchi wameshahama katika eneo hilo, ambapo kwa sasa wanachofanya ni kusafisha eneo hilo kwa kuondoa mapagale, baada ya wananchi kuhama wenyewe kwa hiari yao.

Mkuu huyo wa Wilaya, alisema wananchi waliotakiwa kuhama eneo hilo ni wa Kijiji cha Sanya Stesheni, ambako kuna kaya 596, Tindigani kaya 402 na Chemka kaya 62.

Diwani wa Kata ya KIA, Tehera Mollel, alisema kuwa kazi ya kuwahamisha wananchi waliovamia katika eneo la uwanja na kuweka makazi ilifanyika kwa uaminifu na wananchi wameridhika na fidia waliyopewa.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Loktoli, Daud Sokoine, alisema serikali ilifanya tathimini awali na hakuna mtu yeyote aliyeachwa na baada ya tathimini hiyo serikali imelipa fidia ambapo imewawezesha wananchi kujenga nyumba katika maeneo mengine.

# Wadau walalamika utekelezaji adhabu ya viboko shuleni

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

WADAU wa elimu mkoani Manyara, wamesema takwa la kisheria linalowataka wakuu wa shule za sekondari na msingi, kuruhusu kwa maandishi adhabu ya viboko kwa wanafunzi bado linapuuzwa.

Akizungumzia tatizo hilo jana, Meneja Mradi na Elimu wa Shirika la STC, Grace Swai, alisema licha ya jambo hilo kuwa la kisheria, baadhi ya shule za Mkoa wa Manyara, zinapingana na takwa hilo kwa walimu kuendelea kulazimisha adhabu hiyo kwa kuchapa zaidi ya viboko sita vilivyopendekezwa kisheria.

“Ukimchapa mwanafunzi, unamweka mbali na wewe ili asijifunze zaidi. Wako watoto ambao wanalea familia, wanaishi mbali na shule, ila wakichelewa walimu hawawapi nafasi ya kuwasikiliza wanawachapa zaidi ya vikoko vilivyotajwa kisheria.

“Sasa hii haikubaliki na ndiyo maana tunapaza sauti ili wizara ya kisera inayoshughulika na jambo hili kwa maana ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia walitazame upya na kuwawajibisha wakuu wa shule wanaofumbia macho adhabu hii,”alisema Swai.

Aidha, Ofisa Mradi wa Sauti Yangu wa shirika hilo, Peter Nelson, alisema waliguswa kuanzisha kampeni hiyo ili kuwajengea uwezo wanafunzi kuanzia darasa la awali hadi sekondari ili wazijue haki zao, ikiwamo vitu wanavyovipenda na wasivyovipenda.

Nelson, alisema katika mradi huo wanafunzi wanapata fursa ya kuwataja walimu ambao wanatoa adhabu kali na kuwafanyia ukatili.

Vilevile, alisema walimu zaidi ya 300 wamewapa elimu ya mbinu za kuepuka kuchapa viboko na wanawapa fursa ya kwenda kutembelea shule za mchepuo wa kingereza ili wajifunze namna ya kufundisha bila kutoa adhabu ya viboko shuleni.

Kampeni hiyo inahamasisha, wanafunzi badala ya kuwachapa viboko wapewe adhabu ya kubeba kadi na kunyimwa ruhusa ya kucheza na wenzao, au kuwapatia kazi za kwenda kufanya nyumbani.

Ofisa huyo aliiomba serikali iendelee kutoa mafunzo vyuo vya ualimu na waondoe fikra mgando, kwamba lazima watoe adhabu ya viboko.

Naye, Ofisa Programu wa Shirika la HakiElimu, Godfrey Bonaventura, alisema utafiti walioufanya HakiElimu mwaka 2023, unaonyesha asilimia 89.0 ya wanafunzi wamezoea kuchapwa shuleni na asilimia 10.0 wamezoea kuchapwa nyumbani.

Kadhalika, asilimia 37.1 ya wanafunzi huchapwa na walimu kila siku katika maeneo ya vijijini, huku asilimia 16 wakieleza kuchapwa na walimu mijini kila siku.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA NISHATI**

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)**

ewura

## TAARIFA KWA UMMA

**(Imetolewa chini ya Kifungu Na. 126 cha Sheria ya Petroli, Sura ya 392 na Kanuni Na. 5(1) ya Kanuni za Mafuta (Compressed Natural Gas) (Supply and Marketing Services Rules, GN No. 220 of 2019).**

**TAARIFA** inatolewa kwa Umma kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea ombi la kibali cha ujenzi wa kituo cha kupokea na kupunguza msukumo wa gesi asilia iliyoshindiliwa kwa ajili ya matumizi ya kiwandani kutoka kiwanda cha **GLOBAL ALUMINIUM LIMITED** kilichopo kitalu No. 11, Block “F”, Zegereni Eneo La Viwanda, Mtaa Wa Zegereni, Kata Ya Visiga Wilaya Ya Kibaha , Mkoa Wa Pwani.

Hivyo, mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi dhidi ya ombi tajwa hapo juu, afanye hivyo kwa maandishi na kuwasilisha EWURA kwa anwani iliyotajwa hapa chini ndani ya siku kumi na nne toka tarehe ya tangazo hili.

**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**
**Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA, 41104 Tambukareli**
**S. L. P 2857, Dodoma.**
**Simu: +255-26 2329003-3; Nukushi: +255-26 2329005;**
**Namba ya Bure 0800110030;**
**Barua pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: http.//www.ewura.go.tz**

**Imetolea na:**
**Mkurugenzi Mkuu**
**EWURA**



Lindi Jumbo Limited

# VACANCIES

**About Lindi Jumbo Ltd**

Lindi Jumbo is a Tanzanian graphite mining company developing a high-grade, low-cost mine expected to begin production in early 2024. The company is well-positioned to capitalize on the growing demand for graphite as the world transitions to a clean energy economy. Lindi Jumbo is committed to sustainable mining practices and contributing to the social and economic development of the Lindi Region.


- Operations Manager
- Senior Plant Metallurgist

- **Location: Matambarale, Ruangwa District, Tanzania.**
- **Closing Date: 25 May 2024, 4:00PM (GMT+2)**

SCAN ME

To apply or view more details visit: https://jobportunities.net/jobs_search.aspx or scan the QR Code.

*For assistance on the portal, please contact Lindi Jumbo at +255 616 007 201.*
*Alternatively send an email via the recruitment portal’s Contact Us page.*



# MWAUWASA yaanza kufunga mita za 'luku'

**Na Vitus Audax,** ILEMELA

MAMLAKA ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) imeanza utekelezaji wa agizo la Rais Samia Suluhu Hassan la kufunga mita za maji za malipo ya kabla 'pre-paid' zinazolenga kudhibiti hujuma kwa wateja.

Hayo yamebainishwa juzi na Mkurugenzi wa Usambazi wa mamlaka hiyo, Robert Lupoja, wakati akijibu maswali ya madiwani katika mkutano wa baraza la madiwani uliolenga kujadili taarifa ya utekelezaji wa robo ya tatu kwa kipindi cha Januari hadi Machi mwaka huu.

Lupoja alisema hatua hiyo imeanza kwa majaribio kwa kufunga mita 50 kwa wateja walio maeneo ya mjini kati na kuwa wanaendelea kupata huduma ya maji bila tatizo lolote.

Aidha, alisema baada ya miezi mitatu ya majaribio hayo wataanza kufunga mita hizo katika maeneo mengine ya Jiji la Mwanza ikiwemo Ilemela, hivyo kuomba ushirikiano kutoka kwa madiwani pale utekelezaji katika maeneo yao utakapoanza.

Katika hatua nyingine Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kupitia Meneja wa Wilaya ya Ilemela, Meshack Mabushi lilieleza mpango wake wa kupeleka umeme wa kawaida katika Kisiwa cha Base kilichopo Ziwa Victoria ili kuondoa adha ya upatikanaji umeme inayowakabili wananchi wa kisiwani humo.

Mabushi alisema hayo wakati akijibu maswali ya madiwani juu ya upatikanaji wa umeme kisiwani humo pamoja na mitaa mingine 15 na kueleza kuwa mpango huo utatekelezwa kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA).

Akichangia katika mkutano huo, Mbunge wa Ilemela Angelina Mabula alisema wananchi kisiwani humo wanatumia umeme wa nishati ya jua ambao unawalazimu kulipia Sh.1000 kila siku lakini bado wanapata huduma hiyo kwa saa.

Alisema umeme katika eneo hilo unaosimamiwa na mkandarasi wa umeme jua licha ya wananchi kuulipia Sh.1,000 bado unawashwa kuanzia saa 11 asubuhi na kuzimwa saa 3 usiku hali inayokwamisha shughuli za kila siku.

Meneja Mabushi alisema serikali imeweka mpango wa kupeleka umeme katika kisiwa hicho kupitia REA ili wananchi waanze kupata huduma mapema iwezekanavyo.

"Tunatambua uwepo wa tatizo hilo pamoja na kwenye mitaa mingine 15 juzi tulikuwa Dodoma ambapo kupitia bajeti ya mwaka ujao umewekwa mkakati wa kupeleka umeme kupitia REA licha ya kuwa ni eneo ambalo halipo vijijini," alisema Mabushi.

Aidha, alisema ili kufikisha umeme katika kisiwa hicho unatakiwa waya maji 'Marine Cable' wenye urefu wa km 30, hivyo kabla ya Julai Mosi,2024 mchakato utakuwa umeanza na ikishindikana umeme wa kawaida utapelekwa wa sola kwa gharama nafuu.



Mstahiki Meya wa Manispaa ya Ilemela, Renatus Mulunga akifungua Mkutano wa Baraza la Madiwani wa kipindi cha robo ya tatu ya mwaka 2023/24 kulia ni Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa hiyo Marco Isack. **PICHA: VITUS AUDAX**

# Halmashauri Ilemela yatumia milioni 164/- ulipaji fidia

**Na Vitus Audax,** ILEMELA

HALMASHAURI ya Manispaa ya Ilemela, mkoani Mwanza imetumia Sh.milioni 164.02 kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi wa maeneo mbalimbali katika kipindi cha Januari hadi Machi mwaka huu.

Hayo yamebainishwa jana na Kaimu Mkurugezi wa Manispaa ya Ilemela, Marco Isack wakati akiwasilisha taarifa ya mkurugenzi katika baraza la madiwani kwa kipindi cha robo ya tatu ya mwaka 2023/24.

Marco alisema hatua hiyo ni mwendelezo wa ulipaji fidia kwa wananchi na taasisi zinazoidai manispaa hiyo, lengo likiwa ni kukamilisha madeni yote yaliyopo.

Alitaja waliolipwa fidia hizo kuwa ni pamoja na wananchi wanne katika eneo la Buswelu-Nyamadoke, Buswelu-Busenga na Cocacola ambao wamelipwa Sh.milioni 12.5.

Wengine ni wananchi watano katika eneo la Nyafula, Sangabuye na Lugeye ambao wamelipwa Sh.milioni 16.36.

Wengine ni wananchi wawili katika eneo la viwanda Nyamohongolo ambao walilipwa Sh.milioni nne, Sh.milioni 25.2 kwa mwananchi mmoja katika eneo la Shule ya Nyamanoro.

"Vilevile tumelipa wananchi wanne Sh.milioni 49.972 katika eneo la East Buswelu, Sh.milioni 48.02 imelipwa kwa wananchi wawili katika eneo la Shule ya Sekondari Lumala na Sh.milioni 7.898 kwa wananchi watatu," alisema.

Katika hatua nyingine Marco alisema kuwa hadi kufikia Machi 31, mwaka huu halmashauri hiyo ilikusanya zaidi ya Sh.bilioni 10.144 sawa na asilimia 68 ya makusudio ya bajeti ya ndani.

Vilevile, alisema wametekeleza miradi ya zaidi ya Sh.bilioni 3.9 kutoka serikali kuu ikiwemo miradi ya TASAF na TACTIC, huku katika robo ya tatu zaidi ya Sh.milioni 679 ziliwekezwa katika miradi mbalimbali ya maendeleo.

Akifunga mkutano huo, Mstahiki Meya wa Manispaa hiyo Renatus Mulunga aliwataka madiwani kutoa ushirikiano kwa wakuu wa idara pamoja na wakusanyaji mapato ili kuiwezesha manispaa hiyo kufikia malengo na kufikisha huduma za kijamii ipasavyo.

## Teknolojia yatajwa chanzo ongezeko tatizo afya ya akili

**Na Remmy Moka,** SAUT

UKUAJI wa teknolojia ulimwenguni umetajwa kuwa sababu ya ongezeko la matatizo ya afya ya akili hususani kwa wanafunzi wa vyuo vikuu, hali inayosababisha kuporomoka kitaaluma na kimaadili.

Hayo yalibainishwa na washiriki wa Kongamano la Tatu la Chama cha Ushauri Nasaha Tanzania (TACOGA) katika vyuo vikuu lililowajumuisha washauri kutoka nchi za Afrika Mashariki lililofanyika jijini Mwanza.

Lengo la kongamano hilo ni kujadili masuala mtambuka yanayowakabili wanafunzi wengi wanapokuwa vyuoni na namna ya kutatua changamoto hizo.

Mmojawa wahadhiri kutoka Chuo Kikuu cha Uhasibu Dar es Salaam alisema kutokana na tatizo hilo ni nafasi ya washauri wa wanafunzi vyuoni kuwa chachu katika kukabiliana na tatizo hilo la afya ya akili.

Alisema tatizo hilo husababisha baadhi ya wanafunzi vijana kujiingiza katika vitendo vya matumizi ya dawa za kulevya, ulevi, kulawitiana.

Mhadhiri kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Rhoda Aroko alisema wakati huu wa kukua kwa utandawazi idadi kubwa ya wanafunzi wanaoanza masomo vyuoni ni wale wenye umri mdogo kulinganisha na miaka ya nyuma, jambo linarahisisha wao kujiingiza katika vitendo hivyo bila wao kujua kutokana na akili zao kutokupevuka.

Rhoda alisema athari hiyo imekuwa ikipitiliza zaidi hasa kwenye suala la mahusiano pamoja na ukosefu wa fedha hali ambayo imekuwa ikichochea ongezeko la vijana wenye tatizo la afya ya akili na kusababisha wengine kuacha masomo kwa msongo wa mawazo.

Naye Mwenyekiti wa chama hicho, Sophia Nchimbi aliwataka wanafunzi kushirikisha washauri wao vyuoni pindi matatizo wanapowakabili, kushirikisha changamoto zao na kuzipeleke katika ofisi za washauri katika vyuo wanavyosoma.

Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino (SAUT) Taaluma, Prof. Hosea Rwegoshora aliwataka washauri hao kutumia fursa hiyo ya kongamano katika kuleta tija katika chama hicho cha ushauri kwa wanafunzi.

Nipashe Spotik



WAINGEREZA 6 WANAOWEZA KUUZWA KWA FAIDA KUBWA UK. 12-13



VINICIUS JR

# WACHEZAJI 7 BORA NUSU FAINALI UEFA

## ISIKUPITE

TANGU Real Madrid na Borussia Dortmund zianze kukutana kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya katika hatua mbalimbali kwa mara ya kwanza April 1998, zimekutana mara 14, Dortmund iishinda mara tatu, sare tano huku Madrid ikishinda mara sita. Hata hivyo Cristiano Ronaldo (Madrid), ndiye mchezaji aliyefunga mabao mengi zaidi (saba), akifuatiwa na Robert Lewandowski (Dortmund - 5), Pierre-Emerick Aubameyang (Dortmund - 5), Marco Reus (Dortmund - 4) na Karim Benzema (Real Madrid - 3).



**NYON,** Uswisi

NUSU ainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kila kukicha ilikuwa ya kusisimua, ya kustaajabisha na ya kushtua kama tulivyotarajia ingekuwa.

Wapenzi wa Real Madrid walichelewa kujihakikishia nafasi ya kucheza kwenye Uwanja wa Wembley Jumatano usiku, huku Borussia Dortmund wakiwachabanga Paris Saint-Germain kwa jumla ya mabao 2-0, licha ya miamba hao wa Ligue 1 kugonga nguzo mara 10 kwenye mchezo wa pili wa nusu fainali.

Na baada ya furaha hiyo yote, hawa hapa ni wachezaji saba waliofanya vema katika raundi hiyo...

### 7. Eric Dier

Ikiwa ungemwambia shabiki wa Tottenham kwamba Eric Dier angekuwa mmoja wa wachezaji waliofanya vema katika nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa msimu huu, pengine asingekuelewa.

Kwa kiasi fulani kwa sababu Tottenham hata hawakufuzu kwa michuano hiyo, lakini hasa kwa sababu Dier alikuwa mbaya katika miezi ya hivi karibuni kwa klabu hiyo ya Kaskazini mwa London.

Mnamo Mei 2024 katika nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa, hata hivyo, beki huyo wa kati alikuwa na kipaji kikubwa dhidi ya Real Madrid. Dier aliweka mwili wake kwenye mstari mara nyingi katika miguu yote miwili - kizuizi chake cha kumzuia Brahim Diaz kilikuwa cha kuvutia sana - na alikuwa na bahati mbaya kuwa upande unaopoteza wa Bayern Munich.

### 6. Jadon Sancho

Mchezaji mwingine aliyefanya vema katika nusu fainali msimu huu ni Jadon Sancho.

Baada ya kufukuzwa Manchester na Erik ten Hag, Sancho alikuwa ameendelea kutatizika kupata kiwango bora tangu ahamishwe kwa mkopo Borussia Dortmund hadi wiki iliyopita.

Kisha 2020 Sancho akarudi. Fowadi huyo alikuwa katika hali nzuri kwa BVB katika mechi ya kwanza dhidi ya PSG, akikamilisha chenga 12 za kipuuzi katika ushindi huo kwenye Uwanja wa Signal Iduna Park.

### 5. Toni Kroos

Akiwa na usahihi wa pasi za asilimia 95, na pasi nzuri ya inchi kwa jina lake, ni sawa kusema kwamba Toni Kroos alicheza vema katika nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa msimu huu.

Mjerumani huyo ndiye alikuwa katikati ya safu ya kiungo ya Madrid dhidi ya Bayern, akiweka timu yake kileleni kwa kumiliki mpira kwa ustadi katika miguu yote miwili.

### 4. Nico Schlotterbeck

Kucheza bila kufungwa na Kylian Mbappe ni jambo la kuvutia sana.

Hivyo ndivyo Nico Schlotterbeck alivyoisaidia Borussia Dortmund kufanya katika nusu fainali, akijishikilia dhidi ya baadhi ya washambuliaji bora katika kandanda ya dunia katika dakika zote 180 za hatua kali.

### 3. Joselu

Kutoka Stoke City kwenda kuwa shujaa wa Real Madrid. Hiyo sio njia ya kawaida ya kazi.

Na bado, huyu hapa Joselu - mtu ambaye aliwahi kucheza dhidi ya Stoke City sasa akifunga mabao mawili na kuiwezesha Real Madrid kutinga fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Ni ulimwengu wa ajabu ambao tunaishi.

### 2. Mats Hummels

Akiwa na umri wa miaka 35, Mats Hummels anaweza kuwa ameweka maonesho mawili bora zaidi ya kazi yake ndefu.

Hummels alikuwa wa kipekee kabisa katika safu ya ulinzi ya Dortmund katika miguu yote miwili, na kupata mchezaji bora wa mechi katika michezo yote miwili.

Alifanya vizuri pia katika mechi ya tatu ya mwisho pia, akifunga bao pekee la mkondo wa pili na kuihakikishia Dortmund nafasi ya fainali.

### 1. Vinicius Junior

Kwa kuzingatia jinsi Real Madrid walivyo wazuri na wanacheza michezo mingapi mikubwa, hiyo ndivyo anavyoelewa Vinicius Junior.

Mshambuliaji huyo kwa mara nyingine aliibuka shujaa wa 'Los Blancos' walipomhitaji zaidi, alitoa mabao mawili katika mechi ya kwanza na kumtengenezea Joshua Kimmich katika mkondo wa pili na kuisaidia timu yake kutinga fainali nyingine.

# WAINGEREZA 6 WANAOWEZA KUUZWA KWA FAIDA KUBWA



RASHFORD

**LONDON,** England

WAHASIBU wa Klabu za Ligi Kuu England hufurahi kuwauza wachezaji - na kuzalisha faida nzuri - na kusaidia kufuata sheria kali za kifedha.

**Everton, Nottingham Forest na Leicester City zote zimekumbwa na ukiukaji wa kanuni za fedha huku klabu kama Chelsea, Tottenham, Aston Villa, Newcastle na Wolves zikiwa zimepata hasara kubwa katika akaunti zao za hivi karibuni.**

Baada ya mhitimu wa akademi ya Manchester City, Cole Palmer, kuondoka kwenda Chelsea kwa dili la kushangaza la pauni milioni 42.5 msimu uliopita wa majira ya joto. Je, tunaweza kuona msururu wa uhamisho kama huu msimu huu wa majira ya joto?...

**Conor Gallagher**

Conor Gallagher ana umri wa miaka 24, kiungo wa kati wa Chelsea. Mkataba wake wa mwaka mmoja unamalizika mwishoni mwa msimu. Sokoni anakadiriwa kuwa na thamani ya pauni milioni 68. Anahusishwa na Tottenham.

Kabla ya Cole Palmer kuchukua nafasi ya katikati, unaweza kusema alikuwa ni mchezaji bora wa Chelsea kwa msimu.

Gallagher amechukua nafasi ya nahodha na amekuwa akisifiwa mara kwa mara na kocha Mauricio Pochettino msimu huu.

Uchezaji wa Gallagher umewavutia viongozi waandamizi wa klabu hiyo, hasa ikizingatiwa uwekezaji ambao umefanywa katika nafasi anayocheza kwa kumsajili Enzo Fernandez kwa pauni milioni 106 na dili lenye thamani ya pauni milioni 115 kwa Moises Caicedo.

Mazungumzo kati ya klabu hiyo na wakala wa Gallagher yamekuwa yakiendelea na Gallagher ana furaha klabuni hapo, lakini inafahamika ikiwa ofa ya bei inayostahili itatolewa, Chelsea watakuwa tayari kumuuza.

**Marcus Rashford**

Marcus Rashford mwenye umri wa miaka 26, mshambuliaji wa Manchester United. Alisaini mkataba wa miaka mitano hadi 2028 msimu uliopita. Thamani yake sokoni ikakadiriwa kuwa pauni milioni 85. Anahusishwa kuhamia Paris St-Germain.

Manchester United wako tayari na wazi kuuza mchezaji yeyote katika msimu huu wa majira ya joto, akiwamo Marcus Rashford.

Kampeni ya mwaka jana ya mabao 30 ndiyo iliyomletea mafanikio zaidi, ikifuatiwa na mabao manane pekee msimu huu.

Ana kasi na nguvu ya kumaliza ambayo hutishia mabeki wa timu pinzani. Lakini mara nyingi kiwango chake cha uchezaji hushuka.

Kama mmoja wa wachezaji wanaopata pesa nyingi zaidi United, kiuhalisia soko la Rashford ni dogo. Inaonekana kuna uwezekano mkubwa atabaki Old Trafford.

**Evan Ferguson**

Evan Ferguson mwenye umri wa miaka 19, mchezaji wa mbele wa Brighton. Alitia saini mkataba mpya mwaka jana ambao utakamilika 2029. Thamani yake sokoni inakadiriwa kuwa ni pauni milioni 68. Anahusishwa na Arsenal na Chelsea.

Evan Ferguson alivutia klabu nyingi zilizoongoza msimu uliopita, alipoteuliwa kuwania tuzo ya Mchezaji Bora Chipukizi wa PFA. Ulikuwa msimu wa mafanikio kwa mchezaji huyo wa Kimataifa wa Jamhuri ya Ireland huku Brighton ikifuzu kucheza Kombe la Ulaya kwa mara ya kwanza.

Amefunga mabao sita pekee msimu huu, matatu kati ya hayo aliifunga Newcastle Septemba 2, mwaka jana na safari yake imesita kwa jeraha la kifundo cha mguu.

Hata hivyo, bado anavutia na klabu zote zinazoongoza zinatafuta washambuliaji. Swali kubwa ni, Brighton itakuwa tayari kumuuza ikiwa ada itakuwa nzuri?

**Kiernan Dewsbury-Hall**

Kiernan Dewsbury-Hall mwenye umri wa miaka 25, kiungo wa kati wa Leicester. Ana mkataba hadi 2027. Thamani yake inakadiriwa kuwa pauni milioni 35 sokoni. Anahusishwa kuhamia Brentford, Brighton na Fulham.

Brighton walihusishwa pakubwa kutaka kumnunua Kiernan Dewsbury-Hall Januari mwaka huu, lakini Leicester walishikilia msimamo na kukataa kumuuza walipokuwa wakitafuta kurejea Ligi Kuu. Uhamisho wa Alex Scott wa pauni milioni 25 kwenda Bournemouth kutoka Bristol City mwaka 2023 na uhamisho wa Adam Wharton wa pauni milioni 22 kutoka Blackburn hadi Crystal Palace Januari huenda ukawa ndio viwango vya chini zaidi - lakini kwa kuwa Dewsbury-Hall ana uzoefu wa Ligi Kuu England, Leicester huenda ikahitaji pesa zaidi.

Amefunga mabao 12 katika mechi 44 na kuisaidia Foxes kushinda taji la Uubingwa na kurudi mara moja Ligi Kuu.

Klabu hiyo ilirekodi hasara ya pauni milioni 89 mwaka 2022-23 na tayari imeshtakiwa kwa ukiukaji wa kanuni za faida na uendelevu.

Watahitaji kuwauza wachezaji kabla ya tarehe 30 Juni ili kujaribu kuzuia kutozwa faini mara ya pili 2023-2024 na Dewsbury-Hall ndiye atatoa faida nyingi zaidi.

Kuhusu mchezaji bora wa mwaka katika tuzo za Leicester za mwisho wa msimu Jumanne, Dewsbury-Hall alisema: "Nimekuwa katika klabu hii tangu nikiwa na umri wa miaka minane. Sina nia ya kuondoka."

**Jarrad Branthwaite**

Jarrad Branthwaite mwenye umri wa miaka 21, mlinzi wa Everton. Alisaini mkataba mpya Oktoba mwaka jana ambao utamalizika 2027. Thamani yake sokoni inakadiriwa kuwa pauni milioni 43. Anahusishwa kuhamia Manchester United.

Jarrad Branthwaite alikuwa akiichezea Carlisle United katika Ligi Daraja la Pili akiwa na umri wa miaka 17, kabla ya Everton kulipa pauni milioni moja na kuanza kumkuza katika kikosi chao cha chini ya miaka 23.

Amekuwa muhimu katika msimu mwingine wenye misukosuko kwa Everton kwa kuonyesha utulivu kwenye safu ya ulinzi na kumfanya kuitwa katika kikosi cha England mara kwa mara.

Beki huyo wa kati mwenye kasi na mahiri ameunda ushirikiano mzuri na nahodha James Tarkowski katika kikosi ambacho kimecheza mechi 12 bila kufungwa msimu huu.

Kwa uchezaji wake wa kuvutia kufikia sasa, Branthwaite atalenga kuwa katika kikosi cha wachezaji 26 cha Gareth Southgate na atakuwa katika nafasi ya kuwania mchezaji bora wa Everton.

**Jacob Ramsey**

Jacob Ramsey mwenye umri wa miaka 22, kiungo wa kati wa Aston Villa. Ana mkataba hadi 2027. Thamani yake sokoni inakadiriwa kuwa pauni milioni 34. Anahusishwa kuhamia Newcastle, Bayern Munich au Tottenham.

Jacob Ramsey alishinda tuzo ya akademi ya Ligi ya Kuu Uingereza, msimu uliopita baada ya kufunga mabao sita katika michezo 38, na kuisaidia Villa kurejea katika Ligi ya Ulaya.

Lakini alivunjika uti wa mgongo, jeraha ambalo limemzuia kurudi Ligi Kuu. Villa wamesisitiza hauzwi huku meneja Unai Emery akiweka wazi msimamo wake mwezi Januari.

Emery alisema: "Katika sehemu ya pili ya msimu atakuwa muhimu sana kwetu. Uwezo wake ni wa juu sana, na kiwango cha juu zaidi kuliko matarajio yangu."

Hata hivyo, kumuuza mchezaji huyo kungesaidia klabu katika juhudi zao za kufuata faida baada ya kupoteza pauni milioni 119.6 mwaka ulioshia Mei 31, 2023.

## Nukuu

"Akilini mwangu huwa inanipeleka mahali ambapo tunainua Kombe la Ligi Kuu England. Hapo ndipo akili yangu ilipo kwa sasa. Tunapaswa kuzingatia na kufanya tunachopaswa kufanya ili kuwa katika hali bora zaidi. Hilo ndilo tunalofanya," **Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta, kabla ya kuivaa Manchester United jana.**



"Sijutii kuwa hapa kwa sekunde moja, hii ni klabu kubwa. Hujui changamoto unazopaswa kukabiliana nazo hadi uwe ndani yake. Lakini nilitaka changamoto hii," **Kocha wa Manchester United, Erik ten Hag.**



"Alikuwa na kila kitu, aliweza kupiga chenga, alikimbia nyuma, aliweza kuruka na kupiga mpira kichwa, aliweza kuingia ndani, akatoka nje. Kwa hiyo nasema siku zote alikuwa akinipa wakati mgumju, lakini unajaribuni kufanya kazi kila mmoja nje na tulipata kilicho bora zaidi wakati mwingine," **Beki wa zamani wa Chelsea, Ashley Cole, akielezea kuwa Cristiano Ronaldo, ndiye mshambuliaji aliyempa wakati mgumu zaidi kumkaba katika historia yake ya soka.**





# TIMU TANO ZILIZOSHINDA MECHI NYINGI NYUMBANI

Kikosi cha Yanga ambacho mbali na kuongoza Ligi Kuu, pia kinaongoza kwa kushinda mechi nyingi uwanja wa nyumbani, ambapo kimepata ushindi katika michezo yake yote 13 kilizocheza.

**Na Adam Fungamwango**

LIGI Kuu Tanzania Bara iko ukingoni, huku kila timu ikijitahidi kusaka kile ilichojaaliwa.

**Kuna timu zinazosaka ubingwa na kama zikikosa angalau ziangukie nafasi ya pili na zipo ambazo zinaitafuta nafasi ya nne ambayo inaweza kuzifanya kucheza Kombe la Shirikisho barani Afrika, iwapo bingwa wa Kombe la FA, atamaliza nafasi tatu za juu kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.**

Lipo kundi la timu ambazo zinatafuta pointi tatu kwa ajili ya kujiondoka kabisa katika hatari yoyote ile iwe ya kushuka daraja au kucheza 'play off.'

Halafu kuna timu zipo kwenye vita kamili ya kuwania kutoshuka daraja, hizo hizo ndizo baadhi yao zitashuka na zingine zinaweza kwenda kucheza mechi za mchujo ili kupata nafasi ya mwisho kama zitabaki au la.

Ili kupata yote hayo ni lazima timu ipate ushindi, iwe nyumbani au ugenini. Hata hivyo, kwenye soka, timu nyingi zinatumia sana uwenyeji kushida mechi za nyumbani.

Katika makala haya, tumekusanya takwimu za timu zilizoshinda mechi nyingi zikicheza kwenye viwanja vya nyumbani Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo imefikia raundi ya 26, ikibakisha michezo minne tu kumaliza msimu wa 2023/24...

**5# Prisons (mechi 5)**

Maafande wa Jeshi la Magereza, Prisons, inashika nafasi ya tano kwa timu zilizoshinda mechi nyingi ikicheza uwanja wake wa nyumbani, Sokoine jijini Mbeya. Imeshinda mechi tano, ambazo ni dhidi ya Mtibwa Sugar ikiichapa mabao 3-2, bao 1-0 dhidi ya Dodoma Jiji, ikapata ushindi kama huo dhidi ya Namungo, ikaifunga Singida Fountain Gate 3-1 na Tabora United 2-1.

Timu hiyo imeshinda mechi mbili tu ikicheza ugenini, ikitoa sare 12, na kupoteza mechi saba, ikiwa imeshacheza michezo 26 mpaka sasa. Inashika nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu, ikiwa na pointi 33.

**4# Coastal Union (mechi 7)**

Coastal Union imeshinda michezo saba ikicheza, Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga.

Timu hiyo, inayokamata nafasi ya nne kwenye ligi, imeshinda mechi tatu ugenini, sare saba na kupoteza tisa.

Coastal, yenye pointi 37 mpaka sasa, imeshinda mechi zake nyumbani dhidi ya Mashujaa FC mabao 2-0, ikaifunga Geita Gold 3-1, ikapata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya timu za Kagera Sugar, Dodoma Jiji, Mtibwa Sugar na Ihefu, kabla ya kushinda 2-0 dhidi ya Singida Fountain Gate.

**3# Simba (mechi 8)**

Timu ya Simba inashika nafasi ya tatu kwa kushinda mechi nyingi nyumbani. Msimu huu imetumia viwanja vitatu, ambavyo ni Benjamin Mkapa, Uhuru, na Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam, ambapo mpaka sasa imeshinda mechi nane.

Imeshinda ugenini michezo tisa, kabla ya mechi ya jana dhidi ya Kagera Sugar, ikipoteza tatu na sare tano.

Mechi ambazo Simba imeshinda nyumbani ni dhidi ya Dodoma Jiji, ikipata ushindi wa mabao 2-0, lakini ikapata ushindi kama huo dhidi ya Mashujaa FC, Mtibwa Sugar na Tabora United, ikishinda mabao 3-0 dhidi ya Coastal Union, Kagera Sugar na Azam FC, na kuichapa Singida Fountain Gate 3-1.

**2# Azam FC (mechi 11)**

Licha ya kushika nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi, lakini pia Azam FC, inashika nafasi kama hiyo kwa timu zilizoshinda michezo mingi nyumbani.

Inatumia viwanja viwili, Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam na wakati mwingine, Benjamin Mkapa, kama viwanja vyake vya nyumbani.

Azam imeshinda mechi saba ugenini, ikitoa sare tano na kupoteza tatu, ikiwa imecheza michezo 26.

Imeshinda michezo 11 nyumbani kwa kuzipa kipigo cha mabao 2-0 timu za Yanga, JKT Tanzania na Singida Fountain Gate, ikazifunga KMC na Mtibwa Sugar mabao 5-0 kila moja, ikashinda 4-1 dhidi ya Dodoma Jiji, 4-0 dhidi ya Tabora United na bao 1-0 dhidi ya Ihefu FC.

**1# Yanga (mechi 13)**

Yanga ndiyo timu iliyoshinda mechi zote ilizocheza nyumbani kwa asilimia 100 mpaka sasa. Imecheza mechi 13 nyumbani na kushinda zote. Inatumia Uwanja wa Benjamin Mkapa na Azam Complex, kwa mechi za nyumbani.

Katika mechi 26 ilizocheza, imeshinda tisa ugenini, ikipoteza mbili na sare mbili.

Timu hiyo inayoongoza kwenye msimamo wa ligi, imeshinda mechi zake dhidi ya KMC, Ihefu FC na JKT Tanzania kwa mabao 5-0 kila moja, bao 1-0 dhidi ya Namungo, Dodoma Jiji, Coastal Union, Geita Gold na Kagera Sugar, ambao 2-1 dhidi ya Mashujaa FC na Simba, mabao 3-2 dhidi ya Azam FC na 2-0 dhidi ya Singida Fountain Gate, lakini pia ikichapa Mtibwa Sugar 4-1.

**JE, WAJUA?**

Arsenal na Barcelona, zote zimeingia kwa miguu miwili katika mbio za kuinasa saini ya Kiungo Mkabaji wa Real Sociedad, Mhispania Rtin Zubimendi, kuelekea dirisha la usajili lijalo la majira ya joto.



## TAKUKURU yatoa onyo kuelekea Uchaguzi Serikali za Mitaa

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), mkoani Dodoma imewatahadharisha wagombea uchaguzi wa serikali za mitaa kujiepusha na vitendo vya rushwa kwa wapiga kura, ili taifa lipate viongozi bora.

Mkuu wa TAKUKURU mkoani hapa, John Joseph aliyasema hayo jana kwenye semina kwa waandishi wa habari kwa ajili ya kujiandaa kuripoti habari za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Alisema taasisi hiyo imejipanga kusimamia vyema uchaguzi huo ili uwe huru na haki na kupata viongozi bora kwa ajili ya kuwaongoza wananchi.

"Nawaasa viongozi jiepusheni na vitendo vya rushwa TAKUKURU iko imara kuangalia watoa rushwa na wapokea rushwa,"alisema Joseph.

Alifafanua zaidi ya kuwa kumekuwa na tabia ya kuwarubuni wananchi kwa pesa na bidhaa tofauti, ambapo alisema atakayebainika hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

Kutokana hilo alisema semina iliyotolewa kwa waandishi wa habari ikawe chachu ya kuwaelimisha jamii mbalimbali pale wanapoona kuna viashiria vya rushwa.

Akizungumzia kuhusiana na utoaji elimu kwa jamii, mkuu huyo alisema taasisi hiyo inatoa elimu kwa makundi mbalimbali, wakiwamo wanafunzi wa sekondari mpaka vyuo.

Alisema wanafanya hivyo ili kuona kila jamii inajua nini maana ya rushwa na wanaelewa madhara ya utoaji na upokeaji rushwa.

Hivyo, aliwahimiza waandishi wa habari kujua mipaka yao kwenye kuripoti stori za uchaguzi na wasitumie kalamu zao kurubuniwa na wagombea.

Naye, Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Waandishi wa Habari mkoani Dodoma, Katare Mbashiru aliishukuru TAKUKURU kwa kutoa semina hiyo itakayosaidia kufanya kazi zao kwa ufanisi katika kuandika habari za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

# Miaka mitatu TEMESA yapokea bilioni 7.2/-

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIKA kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) umepokea Sh. bilioni 7.2 kwa ajili ya ujenzi wa karakana mpya na ukarabati.

Kaimu Mtendaji Mkuu wa TEMESA, Josephine Matiro alisema hayo juzi alipokuwa akieleza mafanikio ya wakala huo kwa Mkoa wa Dodoma yaliyopatikana katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita.

Alisema Mkoa wa Dodoma ni mnufaika wa fedha hizo kwa kuwa serikali kupitia TEMESA imeanza mchakato wa usanifu wa karakana mpya na ya kisasa ambayo itajengwa katika maeneo ya Kizota mkoani Dodoma.

"Karakana hiyo inatarajiwa kuwa ya kisasa ambayo itaweza kuhudumia magari yote ya taasisi za serikali mkoani Dodoma kwa ufanisi mkubwa kwa sasa iko katika hatua za usanifu chini ya mtaalamu Chuo Kikuu cha Ardhi" alisema Matiro.

Kuhusu ukarabati wa karakana ya zamani ya Mkoa wa Dodoma, alisema mkandarasi tayari amepatikana ambaye ni M/S Wagerasi Investment Ltd kutoka Dar es Salaam na mkataba umeshasainiwa wa Sh. milioni 973.7 pamoja na VAT.

"Mkandarasi huyo anatarajiwa kuanza kazi muda wowote kuanzia sasa ili kuboresha utoaji huduma katika karakana yetu ya Mkoa wa Dodoma," alisisitiza Matiro.

Aidha, alisema katika kipindi hicho cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia, serikali imetoa zaidi ya Sh. bilioni 1.1 kwa ajili ya kununua vitendea kazi vipya.

"Karakana ya Mkoa wa Dodoma ni miongoni mwa wanufaika karakana ambazo zimefaidika kwa kupata vitendea kazi hivyo vilivyogharimu kiasi cha Sh. milioni 545. 8 ambavyo vinaendelea kutumika na kuongeza ufanisi katika utendaji kazi wa karakana hiyo," alisema.

Kadhalika, alisema wakala pia umekuwa ukiwapeleka kwenye mafunzo wataalamu wake ikiwemo mafundi ili waweze kuendana na mabadiliko ya kiteknolojia yanayoendelea kutokea mara kwa mara kwenye magari.

"Aidha, ili kuendelea kuboresha huduma za karakana Novemba, 2023, timu ya maofisa kutoka TEMESA walishiriki katika mkutano wa ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhusu sekta ya ujenzi.

"Uliofanyika hapa Dodoma ambapo TEMESA na Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Zanzibar waliingia ushirikiano katika kuwajengea uwezo mafundi kuhusu masuala ya ufundi na matengenezo ya magari,"alisema.

Hata hivyo, alisema wakala umetekeleza miradi mbalimbali ya umeme mkoani Dodoma ikiwemo kusanifu na kusimika mifumo ya umeme, mifumo ya TEHAMA na mifumo ya viashiria moto, mifumo ya lifti, kangavuke pamoja na mifumo ya upozaji hewa katika majengo mbalimbali yanayoendelea kujengwa katika makao makuu ya nchi Dodoma.




Naibu Waziri Mkuu, Dk Doto Biteko akikata utepe kuashiria kuzindua rasmi kadi za kidijitali za uanachama wa Chama cha Msalaba Mwekundu Jijini Dodoma mwisho wa wiki wakati wa maadhimisho ya miaka 62 ya chama hicho hapa nchini. Wengine ni Waziri wa Katiba na Sheria Dk Pindi Chana (wapili kulia) na wapili kushoto ni rais wa chama hicho hapa nchini David Kienzile. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Madiwani wapewa jukumu kuhamasisha uchangiaji damu

**Na Thobias Mwanakatwe,**
IRAMBA

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba mkoani Singida wameagizwa kuhamasisha wananchi kuchangia damu kwa hiari, kwani kuna upungufu mkubwa wa damu salama katika hospitali ya wilaya hiyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba, Michael Matomora alitoa wito huo kwenye kikao cha robo ya tatu cha baraza la madiwani kilichofanyika juzi.

Alisema kwa kuwa jamii ndiyo chanzo cha damu na hakuna chanzo kingine, hivyo kuna umuhimu kwa wananchi kwenda kuchangia damu kwenye vituo vya afya na zahanati kwani damu hizo zitawasaidia wao wenyewe watakapohitaji kuongezewa huduma ya damu salama.

"Naomba nitoe taarifa ya hali ya damu salama katika hospitali yetu ya wilaya na vituo vyetu vya afya siyo shwari kwani katika hospitali yetu ya wilaya mpaka asubuhi hii damu salama iliyopo ni chupa 24 tu na tuna chupa 33 pekee za damu ambazo bado zinafanyiwa uchunguzi," alisema.

Mkurugenzi huyo alisena chupa hizo 24 zilizopo za damu salama ni za makundi manne ya damu A, B, AB na O ambazo zote ni positive (hasi) tu.

Alisema damu za kundi la negative (chanya) hakuna hata moja kwani akipatikana mgonjwa au wagonjwa wanaohitaji makundi ya damu hizo itakuwa ni shida.

Katika hatua nyingine Mkuu wa Wilaya ya Manyoni, Kemirembe Lwota, amewataka wananchi kuchukua tahadhari za magonjwa ya milipuko kwa kuchemsha maji ya kunywa na kuzingatia taratibu zote za afya.

Akizungumza na wananchi wa Kata ya Majiri, alisema kutokana na mvua inazonyesha ni vizuri wananchi wakachukua tahadhari za kiafya kwa kunawa mikono vizuri kwa maji tiririka, kujenga vyoo bora na kuvitumia vizuri, kula chakula cha moto lakini pia kuepuka msongamano.





# 'Watendaji Mamlaka ya Bima fuateni maono ya Rais Samia'

**Na Mwandishi Wetu**

WATENDAJI wa Mamlaka ya Bima wametakiwa kufanyia kazi maono ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwa wabunifu na uthubutu.

Wametakiwa kuwa na kasi, kutafakari na kutathmini mbinu na mkakati wa kisera wa kutekeleza maono ya Rais Samia.

Rai hiyo ilimetolewa na Meneja wa Mamlaka ya Bina Kanda ya Magharibi, Dk. Emmanuel Lupilya wakati akizungumza na gazeti hili kuhusu ukuaji na uendelezaji wa soko la bima nchini.

Anasema hatua zilizochukuliwa na watendaji wa mamlaka hiyo akiwemo Kamishna wa Bima, Dk. Baghayo Saqware na Naibu Kamishna wa Bima Khadija Said ni pamoja na kueleweza, kuongoza, kutoa ujuzi mbadala wa kuja na mikakati bunifu ya kutekeleza maelekezo yao.

Dk. Lupilya alisema mamlaka iliandaa miongozo mbalimbali, ikiwemo miongozo ya ulipaji fidia ambayo tayari elimu kwa mifano hai imeanza kutolewa.

Anasema kasi na ufanisi wa kulipa madai bila shurti au kusukumwa, hasa kwa kutumia miongozo itolewayo na mamlaka ni nguzo imara ya kubadilisha imani na uaminifu wa wadau wa bima na soko lake kwa ujumla.

Alisema biashara za bima ni biashara za kulipa fidia, hivyo mamlaka imeweka misingi na mifumo imara ya udhibiti thabiti juu ya malipo ya fidia kwa wadau wa bima pindi wanapopata majanga kwa kuzingatia miongozo iliyo wazi na ya kimaadili.

Dk. Lupilya alisema kwa kutumia mwongozo wa fidia za vifo mtu wa tatu, wasajiliwa au watoa huduma za bima watapata suluhu za kuaminika na salama.

Aidha, alisema uongozi wa Bodi ya Bima ya Taifa, chini ya Mwenyekiti wake Molemi Marwa, amekuwa chachu na kolezo la kuleta mabadiliko kwenye tasnia ya bima.

Kuhusu Kanda ya Magharibi - Tabora, anasema imeendelea kushiriki mikutano mbalimbali ya kimkoa, kiwilaya, na kikata kwa lengo la kuhakikisha kuwa imani na uaminifu katika soko la bima inaongezeka.

Alisema ndani ya miaka miwili mamlaka hiyo imekuwa na mabadiliko kwa kuimarishwa kwa huduma, upatikanaji, utoaji na ulipaji wa fidia kwa wakati, kutokana na huduma za bima kwa Watanzania.

Alisema mamlaka ya bima imeweka timu madhubuti iliyo chini ya uongozi wa Kamishna na Naibu Kamisha, imeendelea kuonyesha ukomavu na weledi uliotukuka katika kusimamia na kutekeleza sheria, miongozo na kanuni za bima.

## Kaya maskini 56 zapokea mbuzi 168

**Na Elizabeth John,** WANGING'OMBE

MBUZI 168 wenye thamani ya Sh. milioni 24.8 wamekabidhiwa kwa kaya 56 za walengwa wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kupitia mradi wa kuongeza kipato cha kaya maskini wilayani Wanging'ombe.

Kaya zinazonufaika na mradi huo ni kutoka vijiji vya Hanjawanu, Igomba na Igelango-Uhambule ikiwa ni moja ya mkakati wa kukabiliana na umasikini.

Akisoma taarifa wakati wa ugawaji wa mbuzi hao, Mtendaji wa Kijiji cha Igomba, Yuda Lulandala alisema mradi huo utawasaidia kuinua vipato vya wanufaika hao kuwandoa katika hali ya umasikini.

Naye Faiza Muhadh aliushukuru TASAF kwa kuwaletea mradi huo akisema utawasaidia kuendesha familia ikiwemo kupeleka watoto shule.

Mkuu wa Wilaya ya Wanging'ombe, Claudia Kitta aliagiza kamati ya usimamizi wa miradi ya jamii kufuatilia mradi huo wa ufugaji ili ulete tija sambamba na kufia lengo lililokusudiwa.

Mratibu wa TASAF Wilaya ya Wanging'ombe, Joyce Mdemwa alisema mradi huo umekuwa na manufaa kwa wanufaika wengi.

"Awali tuligawa mbuzi katika Kijiji cha Hanjawanu Machi mwaka huu lakini mpaka sasa naongea ni kipindi cha mwezi mmoja tu kimepita tayari mbuzi mmoja ameshaanza kuzaa ambapo ni jumla ya kaya sita mbuzi wameongezeka," alisema Mdemwa.

Mdemwa alisema mbuzi hao wamepatiwa dawa za kuongeza vitamini na kinga za magonjwa nyemelezi ili kuhakikisha mifugo hiyo inaendelea kukua katika hali salama na kuendelea kuzaliana.

Alibainisha kuwa serikali kupitia TASAF unatekeleza mradi wa kuongeza kipato uitwao IGA na kila kaya inapewa mbuzi watatu ambapo mmoja dume na wawili jike.

## Migogoro wanandoa chanzo vitendo vya ukatili kwa watoto

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WANANDOA mkoani Njombe wametakiwa kushirikiana katika malezi ya watoto licha ya migogoro inayowakabili ili kuwaepusha na vitendo vya ukatili na mmomonyoko wa maadili.

Wito huo ulitolewa na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Shujaa wa Maendeleo na Ustawi wa Jmii Tanzanni (SMAUJATA) Mkoa wa Njombe, Given Tweve wakati akizungumza na waamini wa Kanisa la Waadventista Wasabato lililopo Mtaa wa Uhuru Halmashauri ya Mji wa Makambako.

Tweve alisema migogoro ya ndoa imekuwa sababu ya watoto wengi kufanyiwa ukatili na kukosa malezi ya baba na mama.

Tweve alisema kitendo cha wanandoa kutengana kinasababisha mtoto akose mtu wa kumueleza changamoto zake hasa pale anapofanyiwa ukatili.

Naye Naibu Katibu wa SMAUJATA Mkoa wa Njombe, Robert Matimbwa alisema vitendo vingi vya ukatili ambavyo watoto wanafanyiwa vinatokana na migogoro ya wanandoa.

Mzee wa kanisa hilo, Ombeni Elihaki aliitaka jamii kuelewa kuwa jukumu kubwa la malezi ya watoto linaanzia kwa wenye ndoa.

Baadhi ya waamini wa kanisa hilo akiwemo Yona Mgohole na Remmy Chodota walisema iko haja ya elimu hiyo kuendelea kutolewa kwa jamii ili kuepukana na vitendo vya ukatili ambavyo vimesababisha athari kubwa kwa watoto, wanawake na baadhi ya wanaume.



Meneja Mkuu wa Mgodi wa Dhahabu wa Barrick North Mara, Apolinary Lyambiko (wa tatu kulia), Meneja Mahusiano ya Jamii, Francis Uhadi (wa pili kushoto) na wafanyakazi wengine wa mgodi huo wakiwa na Mratibu wa Miradi wa Shirika la People Development Forum (PDF) Tanzania, Rose Nazarya (wa tatu kulia) wakikabidhi hundi ya Dola za Marekani 10,000 kwa taasisi hiyo kwa ajili ya kutoa elimu juu ya madhara ya ukeketaji. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Majaliwa: Tathimini uharibifu barabara, madaraja inaendelea

**Na Nebart Msokwa,** BUSOKELO

SERIKALI imesema inaendelea kufanya tathimini ya uharibifu wa barabara na madaraja uliosababishwa na mafuriko yaliyotokea katika maeneo mbalimbali nchini na kuendelea kurejesha mawasiliano.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa aliyasema hayo juzi alipozungumza na wananchi wa Halmashauri ya Busokelo mkoani Mbeya alipofanya ziara ya kukagua miradi ya maendeleo likiwemo jengo la halmashauri hiyo.

Alisema barabara nyingi nchini zimekatika kutokana na mafuriko ambayo yamesababishwa na mvua iliyonyesha juu ya wastani kuanzia Oktoba mwaka jana mpaka sasa.

Alisema baadhi ya barabara zilizoharibika ni zile zinazotumika na wananchi kwenye maeneo yao kusafirisha mazao, zinazounganisha wilaya, mikoa.

Majaliwa alisema kati ya barabara muhimu ambazo zimekatika ni inayounganisha mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma na Dar es salaam.

"Moja ya maeneo iliyokatika barabara hiyo lina urefu wa zaidi ya mita 200, Waziri wa Ujenzi alikuwa huko na mpaka sasa tumeshafanikiwa kurejesha mawasiliano kwa kujaza kifusi ili mabasi yapite na wananchi waendelee na majukumu yao," alisema Majaliwa.Waziri Mkuu alisema uharibifu huo ulisababisha serikali kusimamisha baadhi ya miradi mipya ili kurejesha mawasiliano kwenye maeneo yaliyoathirika.

Alisema tathimini inaendelea kufanyika kwenye maeneo ambayo barabara zimesombwa na mafuriko ili kubaini kama yanahitajika kujengwa madaraja ama kuendelea kujengwa kwa kiwango cha lami.

Hivyo aliwahakikishia wananchi wa Busokelo kuwa serikali itaendelea kujenga miundombinu mipya kwenye halmashauri hiyo zikiwemo nyumba za watumishi.

Alisema serikali itahakikisha inakamilisha ujenzi wa jengo la halmashauri hiyo ambalo limekamilika kwa asilimia 94.7 ili watumishi wafanye kazi ya kuwahudumia wananchi vile inavyostahili.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Busokelo, Loema Peter alisema walianza kujenga jengo hilo mwaka 2013 kwa kutumia makandarasi ambao mpaka mwaka 2020 walikuwa wamejenga kwa asilimia 35 pekee.

Alisema baada ya hapo waliamua kutumia mfumo wa mafundi wa mitaani ambao walikuwa wanasimamiwa na Kitengo cha Ukandarasi cha Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST).

Alisema jengo hilo limejengwa kwa Sh. bilioni sita na kwamba makisio yaliyofanywa na Chuo cha MUST yamebaini kuwa zinahitajika Sh. bilioni 2.4 ili kukamilisha maeneo yaliyobakia.



## Watakiwa kuacha uvuvi haramu ili kuokoa kizazi kijacho

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Shaaban Ali Othman amewataka wavuvi wa Unguja na Pemba kuachana na uvuvi haramu kwa ajili ya maslahi ya sasa na kizazi cha baadae.

Alitoa onyo hilo juzi wakati wa kikao na wavuvi wa eneo la Chakwa Wilaya ya Kati Unguja.

Waziri Shaabani alisema serikali inachukua jitihada ya kuwawezesha wavuvi ikiwemo kuwapatia mikopo nafuu ya boti zikiwa na nyavu zinazokubalika kisheria ili kuondokana na uvuvi haramu nchini.

"Lazima tufikie mahali uvuvi haramu tuachane nao ili tuende sambamba na matakwa ya serikali "alisema.

Aidha aliwataka wavuvi wa Kijiji cha Chwaka kuwa wamoja na kutafuta mbadala wa kuachana na uvuvi haramu ili serikali ione namna ya kuwasaidia.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kati Unguja, Sadifa Juma Khamis aliwata wavuvi hao kufuata sheria ili kuepusha migongano kati ya serikali na wananchi.

Mkurugenzi wa Uhifadhi wa Bahari, Dk. Makame Omar Makame alisema Sheria ya Uvuvi Namba 7 ya Mwaka 2010 imeweka wazi kukataza matumizi ya nyavu za kukokota katika maeneo tengefu pasipo kuruhusiwa na taasisi husika.

Kadhalika, wavuvi wa kijiji hicho waliitaka serikali kuwapatia fidia ya vyombo vyao wanavyotumia kwa uvuvi haramu, ili waachane na uvuvi huo na kuvua uvuvi unaokubalika kisheria.

# UWT watakiwa kuzingatia mafunzo, kukijenga chama

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla ameutaka uongozi wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) na wanachama wake kuyatumia vyema mafunzo wanayopewa ili kukisaidia Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Amesema mafunzo hayo yatawajengea uwezo wa utekelezaji wa majukumu na kuleta mabadiliko ya kiutendaji katika CCM sambamba na kutatua changamoto za wanachama zinapojitokeza.

Alitoa wito huo juzi wakati akifungua semina ya kuwaongezea ujuzi na maarifa madiwani, makatibu wa wadi na majimbo pamoja na wajumbe wa kamati tendaji wa chama hicho.

Hemed alisema moja ya jukumu la UWT ni kutoa elimu kwa wanachama, kuwahamasisha wanawake katika kugombea nafasi za uongozi, kuishauri Serikali na kutatua changamoto katika jamii kwa lengo la kuweka mustakbali mwema wa Taifa na CCM ili kiendelee kushika dola awamu kwa awamu.

Aidha, aliwataka viongozi kuzitumia vyema nafasi zao kwa kufuata misingi ya uongozi kwa wanowaongoza ikiwemo nidhamu, uaminifu, uadilifu, unyenyekevu, kujenga umoja, matumizi mazuri ya lugha, kutatua kero na kuandaa viongozi wapya watakaoweza kushika nafasi katika jumuia.

Alisema anatambua kuwa wapo baadhi ya viongozi na watendaji ambao hawana lugha nzuri kwa wanaowaongoza, hivyo aliwataka kujirekebisha na kuachana na tabia hiyo.

Alisema CCM haitamvumilia mtu yoyote atakayekwenda kinyume na maadili ya chama, huku akiwataka wanawake wenye uwezo wa kuongoza kujiandaa na kujitokeza kugombea katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.

Mwenyekiti wa UWT Taifa, Mary Pius Chatanda, alizipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kukamilisha vyema na kwa mafanikio makubwa Sensa ya Watu na Makazi akisema takwimu zake zitalisaidia Taifa katika kupanga mikakati ya kimaendeleo nchini.

Chatanda aliwataka viongozi ambao wamepatiwa mafunzo hayo kushuka kwa wananchi kusikiliza kero zao ili kufanya maamuzi sahihi katika vikao vya chama na Serikali.

Aidha, aliwataka viongozi wa UWT kuendelea kufanya usajili wa wanachama wapya kwa njia ya kielektroniki ambao watasaidia katika kupanga mikakati ya jumuiya sambamba na kuhakikisha CCM kinashinda kwa kishindo kikubwa katika Uchaguzi Mkuu mwakani.

Makamu Mwenyekiti wa UWT Taifa, Zainab Khamis Shomari, alisema kuwa mafunzo hayo yataleta mabadiliko chanya katika utendaji kazi wa jumuiya na chama.




Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Tabia Maulid Mwita akizungumza na Waandishi wa Habari wa vyombo mbalimbali kuhusiana na Mapokezi ya Mwenge wa Uhuru ambao utawasili Zanzibar katika Kisiwa cha Pemba leo na Unguja Tarehe 17 Mei ukiwa na kauli mbiu isemayo "Tunza Mazingira na Shiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa Ujenzi wa Taifa Endelevu" hafla iliyofanyika katika ukumbi wa Wizara hiyo Migombani Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# ZIPA yatoa vibali vya ukazi kwa wageni wanne

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAMLAKA ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) imetoa vibali vya ukaazi daraja C11 kwa wageni walionunua nyumba katika miradi iliyoidhinishwa na mamlaka hiyo visiwani hapa.

Akikabidhi vibali hivyo katika Ofisi za ZIPA, Kaimu Mkurugenzi wa ZIPA, Yahya Vuai Lada, alisema mamlaka hiyo itaendelea kutoa vibali vya ukaazi kwa wageni ambao watakidhi vigezo vilivyowekwa kisheria.

Alisema mamlaka hiyo inatarajia kupata waombaji wengi ambao watakidhi vigezo vya kisheria kutokana na miradi ya uwekezaji wa nyumba za biashara bado inaendelea.

Alisema kwa mujibu wa Sheria ya Uwekezaji Nambari 10 ya Mwaka 2023, Serikali iliweka kivutio hicho kwa ajili ya kutangaza biashara hiyo pamoja na kueka vigezo tofauti kwa muombaji ili apate kibali na kupeleka kubadilika kwa baadhi ya vipengele vya sheria na kanuni za uhamiaji.

"Leo tunafuraha kuwa na waombaji wa mwanzo ambao tutawapatia vitambulisho vya ukaazi na hii tunaifanya makusudi kwa ajili ya kutimiza ile ahadi ya Serikali," alisema.

Aidha, alisema ahadi hiyo imechukua muda kidogo kutekelezeka kutokana na kuhitaji mchakato ambao utawaondoshea usumbufu wageni watakaonunua nyumba hizo.

Alisema kufanyika kwa kitendo hicho kumetokana na ushirikiano baina ya taasisi tofauti ikiwemo Idara ya Uhamiaji baada ya kufahamu dhamira yao italeta manufaa makubwa kiuchumi na kijamii nchini.

Naye Mfawidhi wa Uhamiaji wa Kituo cha ZIPA, Zakia Kisiri, alisema kutolewa vibali hivyo kumetokana na umuhimu wa kukuza uchumi na kurekebisha Sheria Namba 54 kwa ajili kukidhi haja kwa wale wote waliowekeza kununua nyumba nchini.

Alisema vibali vilivyotolewa ni kwa ajili ya wale ambao hawajakidhi kupata vibali vyengine ambavyo hupewa wawekezaji au wale waliokuja kuajiriwa.

Alisema vibali vilivyotolewa ni kwa ajaili ya makaazi pekee na sio kufanya biashara wala kuekeza kutokana na wanunuzi wa nyumba hizo hawawezi kununua nyumba za kuishi.

Miongoni mwa wanunuaji wa nyumba hizo, Petra Van Der Hagen, kutoka nchini Uholanzi alisema amefurahi baada ya taasisi mbili hizo kumkabidhi kibali hicho cha ukaazi.

Alisema kwamba amekua akisubiria kwa muda wa miaka miwili, jambo ambalo hapo awali alikua akiona ugumu kutokana na kuwa tayari ameshanunua nyumba hiyo.

"Nimefurahi sana mimi na wenzangu wote tulipata vibali vya ukaazi hapa nchini na tumeona kwamba Serikali ya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla inajali na kuthamini wananchi na wageni ambao hufika hapa nchini," alisema.

Petra alisema anaamini ZIPA kwa kushirikiana na taasisi mbali mbali za Serikali itaweza kuwawekea mazingira mazuri na yalio bora wageni ambao wananunua nyumba nchini.

ZIPA kwa kushirikiana na Idara ya Uhamiaji imewakabidhi wageni wanne vibali vva ukaazi daraja la C 11 baada ya kununua nyumba katika eneo la Fumba Wilaya ya Magharibi 'B' Unguja.

# Mpango ashtushwa wimbi la vijana tegemezi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango ameshtushwa na wimbi la vijana tegemezi na kuwataka kutochagua kazi ili wajikwamue kimaisha.

Aidha, amewaomba viongozi wa dini kuutetea ukweli kwa maslahi ya wananchi kwa uhuru bila woga, huku akiwapa angalizo kutoathiri amani na umoja wa kitaifa.

Akizungumza jana jijini hapa kwenye adhimisho la misa ya daraja takatifu la Uaskofu na kuwekwa wakfu Askofu Msaidizi, Wilboard Kibozi wa Jimbo Kuu Katoliki Dodoma, Dk. Mpango alisema hivi sasa kazi nyingi za staha zipo kwenye kilimo cha mboga na matunda, ufugaji wa wanyama na inahitaji nidhamu ya kazi na kujituma.

“Baba wa Taifa alisema kazi ni kipimo cha utu na alisisitiza Watanzania kufanya kazi ili kujipatia kipato kwa njia halali, hivi sasa wapo vijana wengi wenye umri wa kufanya kazi, lakini hawajishughulishi na kazi yoyote ili kujikimu kimaisha na wamekuwa wategemezi,” alisema.

Kuhusu malezi na makuzi ya watoto, alisema inasababishwa na mambo mengi, ikiwamo matumizi mabaya ya maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano na mwingiliano wa mila na desturi za mataifa mbalimbali.

“Moja ya matokeo hasi ya matumizi ya TEHAMA ni kudhoofika kwa muunganiko wa kindugu au kirafiki kati ya wazazi au walezi na watoto wao ambao umesababisha watoto kukosa upendo na ulinzi wa wazazi au walezi,” alisema.

Vile vile, alisema ukatili wa mitandao ambao watoto wanarubuniwa kujihusisha na vitendo viovu na kuomba wazazi na walezi kutenga muda wa kujenga urafiki na watoto ili kufahamu maendeleo yao, marafiki wao na kuwawezesha kuwa huru kueleza vikwazo wanavyopitia ili kuwasaidia mapema.

“Malezi kwa watoto ni muhimu sana katika kujenga taifa bora na lenye ustawi, hapa wamekuja watoto wa utatu mtakatifu wameimba vizuri, lakini nimehesabu pale watoto wa kiume wapo watatu tu.”

“Hapa Mhashamu Askofu Kibozi, lile jukumu ulilokabidhiwa ni mzigo kweli, nawaomba sana Watanzania, Wakatoliki tuweke nguvu ya pekee katika malezi na makuzi kwa watoto wote, watoto wa kiume Mungu anatujalia tuwalete hapa nao washiriki na kukua ndani ya kanisa,” alisema.

Kadhalika, alisema Watanzania wengi hawathamini muda na kuutumia vibaya na kwamba ni rasilimali muhimu ikichezewa haiwezi kurejeshwa.

Aliwaomba viongozi wa dini kuhamasisha usafi, upandaji miti na kutunza mazingira bila kuchoka na kukemea utupaji ovyo wa taka, uchombaji misitu na ukataji ovyo wa miti hasa kwa kutumia misumeno ya mnyororo ambayo imekuwa silaha mbaya ya kuangamiza misitu.

“Nakumbusha nyumba za watawa, shule ambazo zinalisha watu 100 kwa siku waanze hatua ya kuhama kutoka matumizi ya nishati chafu na kuanza kutumia nishati safi ili kufikia lengo la taifa ifikapo mwaka 2034 asilimia 80 ya Watanzania wawe wanatumia nishati safi ya kupikia,” alisema.

Alilishukuru kanisa kwa kutoa huduma bora kwa Watanzania bila ubaguzi hasa sekta ya afya, elimu na malezi kwa vijana.

Alisema serikali itaendelea kulinda haki ya kuabudu kwa wananchi na wataishi kwa mazingira ya amani.

“Serikali itaendelea kuunga mkono mashirika ya dini kutoa huduma kwa jamii, hivi sasa tunashughulikia ombi la msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye mradi wa jengo la mama na mtoto Hospitali ya Mtakatifu Gemma,” alisema.

# Zamu Wizara za Afya, Mambo ya Ndani, Uvuvi na Habari bungeni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKUTANO wa Bunge la Bajeti unaendelea na vikao vyake jijini Dodoma. Leo ni zamu ya Wizara ya Afya, ugharamiaji huduma za afya ukitarajiwa ‘kuteka’ mjadala.

Kwa mujibu wa ratiba ya Bunge iliyofanyiwa marekebisho mwishoni mwa wiki, wizara zingine zitakazosomwa wiki hii ni pamoja na ya Mifugo na Uvuvi ambayo itaeleza mageuzi ya uvuvi na ufugaji samaki kupitia wanawake na vijana na ustawi wa sekta ya mifugo.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi itafuata, ikitarajiwa kueleza mikakati yake ya kuimarisha masuala ya ulinzi na usalama ikiwamo kuanza kwa mchakato wa matumizi ya majaketi yenye kamera kwa askari wa usalama barabarani.

Katika Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, mambo yatakayoguswa ni pamoja na ujenzi wa minara ya simu na ukuzaji matumizi ya teknolojia ya akili bandia huku Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ikiratajiwa kugusia maandalizi ya michuano ya AFCON 2027.

Akizungumza kuhusu hotuba ya bajeti ya mapato na matumizi ya Wizara ya Afya, Ofisa Habari wa Wizara hiyo, Englibert Kayombo, alisema Waziri Ummy Mwalimu atawasilisha bungeni leo na kueleza mikakati kabambe ya kuboresha huduma za afya nchini.

Kayombo aliibainisha kuwa katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais  Samia Suluhu Hassan, mageuzi makubwa yamefanyika ndani ya sekta ya afya kwa kushirikiana na wadau wa sekta.

“Ndani ya miaka mitatu bajeti ya afya nchini imeendelea kuimarika, hii inaonesha dhamira ya dhati ya Rais Samia ya kuboresha huduma za afya nchini.

“Mwaka 2021/22, bajeti ya afya ilikuwa ni Sh. trilioni 1.03, mwaka 2022/23 ilikuwa Sh. trilioni 1.1 huku kwa mwaka huu 2023/24 bajeti iliyoidhinishwa na Bunge ilikuwa ni Sh. trilioni 1.23,” alisema.

Ofisa huyo alisema vipaumbele vya Wizara ya Afya kuelekea mwaka mpya wa bajeti ni kuboresha huduma za afya pamoja na masuala ya ugharamiaji huduma za matibabu nchini.


**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 10200 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE NEEMA JOSIA MWANGA**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY CUSBERTI JOSIA MWANGA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)**

ALL PERSON claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 3rd day of June 2024

Dated at Korogwe this 08th day of May 2024

RESIDENT MAGISTRATE
KOROGWE

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

Ndugu **FARAHAN ALLY BILAL** anatangaza kupotelewa na kadi zake za pikipiki zenye aina, usajili na Chassis namba kama ifuatavyo:
**MC 620 BGV KINGLION** yenye chassis Na. **LBMPCJL85H1000614**
**MC 922 CEX KINGLION** yenye chassis Na. **LTBPK8BG6K2K00547**
**MC 827 BNT KINGLION** yenye chassis Na. **LTBPK8BG6G2K16058**
Kwa yeyote atakayeziona anaombwa kutoa taarifa kituo chochote cha Polisi kilicho karibu.
Taarifa Polisi:
**PHQ/TAN/TAN/4298/2024**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA YA MOROGORO**

**KITUO CHA MJINI**
**MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na...24/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: AHAMADI SAIDI NAMGONGO wa MKWAJUNI KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA VUMILIA HASSANI CHUMA**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 7 Mwezi 6 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo Tarehe 7 mwezi 5 mwaka 2024

Hakimu

**FORM 58**

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**

**AT ONE STOP CENTRE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 9582 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE FRANK ROCKY MATTABA**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY AGNES JOHN MWITA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of Administration) is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 18th day of JUNE 2024

Dated at DAR ES SALAAM this 09th day of May 2024

Senior Resident Magistrate

## KUPOTEA KWA CHETI



**EVA AYUBU MWAKOSYA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1492-0011** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **SHULE YA KYEJO SEKONDARI** mwaka 2013. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/MOR/KIL/12495/2024**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**

**IN THE DISTRICT DELEGATE COURT OF MOROGORO AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No 9665 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE ABEL STEPHANO MDULU**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR A LETTER OF ADMINISTRATION BY:-**

**1: FLORA NTANDU KIRUU**
**2: ____________________**

All persons claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above - named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 29 day of May 2024
DATED at MOROGORO this 06 day of May 2024

Resident Magistrate

## KUPOTEA KWA CHETI



**WILLIAM NJARITA KIGOGO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S3661/0146** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **BEROYA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2019. Kwa yeyote atakeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA : **SOG/RB/3748/2023**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

Ndugu **FARAHAN ALLY BILAL** anatangaza kupotelewa na kadi zake za pikipiki zenye aina, usajili na Chassis namba kama ifuatavyo:
**MC 674 BSN KINGLION** yenye chassis Na. **LTBPK8BG8G2K07457**
**MC 723 AXZ SOUND** yenye chassis Na. **LXAPCKRA2CC001163**
Kwa yeyote atakayeziona anaombwa kutoa taarifa kituo chochote cha Polisi kilicho karibu.
Taarifa Polisi:
**PHQ/TAN/TAN/4300/2024**

# 10 wafariki baada ya ushindi wa Mahamat

**N'DJAMENA,** Chad

VYANZO kadhaa vimebainisha kuwa risasi zilizofyatuliwa usiku kusherehekea ushindi wa Mahamat Deby katika uchaguzi wa rais nchini Chad zimesababisha vifo vya watu 10 na kadhaa kujeruhiwa.

Ilielezwa jana kuwa tukio hilo lilitokea usiku wa kudamkia juzi, huku ikibainisha kwamba Wizara ya Afya ya Chad kwa sasa inazuia hospitali kutoa taarifa kwa waandishi wa habari, jambo ambalo limevikasirisha vyama vya waandishi nchini humo.

**Kuhusu ufyatuaji risasi kwa furaha, waziri anatambua kwamba walikuwa na furaha ya kupindukia na anasema anachukizwa na hali hii.**

Uongozi wa vyombo vya habari wa Chad ulieleza kusikitika kwake na kulaani tishio kubwa kwa uhuru wa vyombo vya habari na Umoja wa Waandishi wa Habari wa Chad ulizungumza juu ya kizuizi kwa haki ya umma ya kupata habari.

Katika suala hilo, waraka kutoka Wizara ya Afya unaokataza hospitali kutoa taarifa kwa waandishi wa habari kuhusu majeruhi na waliofariki kutokana na ufyatuaji risasi zilizorushwa na askari na raia wenye silaha baada ya kutangazwa kwa matokeo ya muda ya uchaguzi wa urais licha ya maelekezo ya makao makuu ya jeshi na Wizara ya Usalama wa Umma.

Kwa mujibu wa vyombo vya habari vya ndani na wanaharakati wa mashirika ya kiraia waliohojiwa na RFI, watu watatu walijeruhiwa katika mji wa mpakani wa Kousseri, upande wa Cameroon.

Waraka uliotolewa na wizara ulinukuliwa ukisema "Waziri Abderaman Koulamallah, msemaji wa serikali, anaomba hospitali kutothubutu kutoa habari kwa waandishi wa habari na kuwa na utu heshima kwa binadamu.

"Watu wanaojikubali wanaweza kujieleza vizuri, lakini siri ya matibabu inakataza wafanyakazi wa afya kutoa habari juu ya afya ya wagonjwa, kabla ya kukumbusha kuwa ni marufuku kunasa picha au video hospitalini bila idhini.

"Kuhusu ufyatuaji risasi kwa furaha, waziri anatambua kwamba walikuwa na furaha ya kupindukia na anasema anachukizwa na hali hii. Wanajeshi wameshikamana sana na rais wao ambaye pia ni jenerali. Msemaji wa serikali anaahidi kutoa idadi kamili ya vifo na majeruhi katika saa 24 zijazo," ulisema waraka huo. **RFI**



Wapalestina wanaokimbia mapigano wakiwasili mji wa Khan Younis wakitokea mji wa Rafah walipokimbilia mwanzo kujinusuru na vita, jana. **PICHA: MTANDAO**

## Kilio intaneti kusuasua, TCRA yaanika tatizo

**Na Jenifer Gilla**

WATUMIAJI intaneti jana walijikuta katika wakati mgumu kuanzia saa tano asubuhi baada ya huduma hiyo kusuasua.

Baadhi ya mitandao ya kijamii ilishindwa kufanyakazi inavyotakiwa na kuchukua muda mrefu mithili ya nchi ambayo bado iko kwenye 2G ilhali sasa tupo 5G.

Jana jioni Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, alitoa ufafanuzi kuwa kukosekana kwa huduma hiyo pamoja na huduma za simu kimataifa kulitokana na hitilafu kwenye nyaya zilizoko baharini kati ya Msumbiji na Afrika Kusini.

Alisema walipokea taarifa za awali kutoka kwa kampuni ya Seacom na EASSY kuwa tatizo la nyaya kati ya Msumbiji na Afrika Kusini limesababisha kukosekana kwa huduma hiyo nchini.

"Mnamo majira ya saa tano asubuhi, tumeshuhudia kukosekana kwa huduma za intaneti pamoja na huduma za kimataifa," alisema Nape.

Alisema wakati serikali ikiendelea na jitihaza za kutatua tatizo hilo upatikanaji huduma za intanet na simu za kimataifa utakuwa wa kiwango cha chini kwa kutumia njia mbadala.

Mkurugenzi Mkuu TCRA, Dk. Jabir Bakari alisema tatizo hilo ni la kiufundi linalohusiana na kebo za baharini na kuwa wanaendelea kufuatilia kujua tatizo lilipo na kulifanyia kazi.

Happyness Nyambuya, Mkazi wa Mbezi, Dar es Salaam alidhani kuwa mtandao anaotumia ndio wenye shida huku akihama kutoka sehemu moja hadi nyingine kutafuta mtandao.

Alisema hali hiyo iliendelea hadi saa tano asubuhi hadi pale dada yake alipomweleza kuwa tatizo hilo halipo kwenye mtandao anaotumia tu, bali ni mitandao yote Tanzania.

Mkazi wa Korogwe, Tanga, Florah John, alisema siku ya jana ilikuwa ngumu kwake kwa kuwa alizoea kuingia mitandaoni kuangalia yanayojiri ikiwamo habari za burudani na michezo.

## Aokolewa baada ya siku tano chini ya kifusi

**CAPE TOWN,** Afrika Kusini

MKUU wa shughuli za uokoaji katika jimbo la George nchini Afrika Kusini Colin Deiner amesema wamefanikiwa kumuokoa manusura mmoja baada ya kukaa chini ya kifusi kwa siku tano.

Siku chache zilizopita nchini Afrika Kusini kulitokea ajali ya kuporomoka kwa jengo la ghorofa katika mji wa George, ajali iliyosababisha vifo kwa watu 13, miongoni mwa wafanyakazi 81 waliokuwa eneo la ujenzi.

Akizungumzia kuhusu manusura huyo Mkuu wa jimbo hiyo Alan Winde, kupitia ukurasa wake wa X (zamani twitter) alisema mafanikia hayo ni muujiza ambao wote wamekuwa wakiutarajia kutokea.

Mkuu wa uokoaji Deiner alisema "Tuliposhuka chini ya kifusi ambacho hatukuwa tumekiona, tulisikia mtu ndani na tukasimamisha shughuli zote kubwa, waokoaji walimuita manusura huyo na akajibu".

Alisema baada ya manusura huyo kujibu walianza shughuli ya kumtoa chini ya kifusi hicho, na kufanikiwa kumpata akiwa salama. **VOA**

## Serikali: Tutalinda wenye ualibino dhidi ya ukatili

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA

SERIKALI imesema itaendelea kuchukua hatua za dhati kulinda watu wenye ualbino ikiwamo kuwafikisha katika vyombo vya dola watakaobainika kuwafanyia ukatili.

Hayo yalibainishwa jana na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu – Bunge, Sera na Uratibu, Ummy Nderiananga kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Deogratius Ndejembi kufuatia tukio la shambulio la mtoto mwenye ualbino lililotokea Mei 4, mwaka huu katika Kijiji cha Mtakuja, Katoro, mkoani Geita.

Ummy alisema serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan inakemea kitendo hicho kisichokuwa na utu na inawaomba wananchi kusaidia kudhibiti vitendo hivyo kwa kuimarisha ulinzi ndani ya familia na jamii inayowazunguka.

Vilevile, Ummy alizitaka Kamati za Ulinzi na Usalama nchini kuhakikisha vitendo vya aina hiyo vinadhibitiwa. Ofisi ya Waziri Mkuu itaendelea kushirikiana na Chama cha Watu Wenye Ualbino Tanzania (TAS) kuelimisha jamii kuhusu haki za kundi hilo.

Ummy pia alitoa pole kwa familia ya mtoto Kazungu Malecha (mwenye ualbino) kwa shambulio hilo lililotokea. Ofisi yake imefanya mawasiliano na Wizara ya Elimu kwa ajili ya mtoto huyo kusomea shule ya bweni.

HABARI MICHEZO

# MUDATHIR AWEKA REKODI YA KUAMUA MECHI ZA YANGA SC

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mkabaji wa Yanga, Mudathir Yahaya ameweka rekodi ya aina yake, kwa mabao yake kuipa ushindi na kuamua mechi, katika michezo minne ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

**Jumatano iliyopita, Uwanja wa Azam Complex, alifunga bao pekee dhidi ya Kagera Sugar, ambalo liliipa Yanga pointi tatu katika mchezo huo, na kuweka rekodi ya kuchangia pointi 12 kwa timu yake, katika mabao aliyofunga.**

Mchezaji huyo ambaye ametimiza mabao tisa mpaka sasa, manne kati ya hayo yaliamua matokeo ya mechi, huku mengine matano akifunga katika mechi ambazo wachezaji wenzake wameshafunga, hivyo kuchangia tu ushindi na idadi ya mabao.

"Nafunga kwa sababu kocha Miguel Gamondi ananipa uhuru uwanjani. Mimi ni kiungo mkabaji, lakini huwa anamwambia Khalid Aucho akae nyuma asisogee sana mbele, halafu mimi nakaba, lakini ananiambia niwe nakwenda mbele kusaidia wakati tunashambulia kwa sababu naweza kukutana na mpira nikafunga, na ndivyo inavyokuwa," alisema mchezaji huyo wa Zanzibar Heroes na Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars.

Kwa mujibu wa kitengo chetu cha takwimu, Mudathir alianza kuibeba Yanga, Septemba 20, mwaka jana, alipopachika bao pekee dakika ya 87, timu yake ikishinda 1-0 dhidi ya Namungo FC, Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam, Februari 5, mwaka huu, alifunga bao pekee kwenye uwanja huo huo, dakika ya 85, timu yake ikatoka na ushindi wa 1-0 dhidi ya Dodoma Jiji FC.

Alifunga bao la pili, dakika ya 85, katika uwanja huo huo lililoipa Yanga pointi tatu na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Mashujaa FC, Februari 8, mwaka huu, kabla ya Jumatano iliyopita kufunga bao pekee dakika ya 82 kwenye uwanja huo huo wa Azam Complex, dhidi ya Kagera Sugar, lililoipa pointi tatu muhimu kuelekea kutwaa ubingwa wa Tanzania Bara kwa mara ya tatu mfululizo.

Mbali na mechi hizo, Mudathir amechangia mabao katika mechi kadhaa za Ligi Kuu, ikiwamo ile ya mabao 5-0 dhidi ya KMC iliyochezwa Agosti 23, mwaka jana, akifunga bao moja, lingine katika ushindi wa 3-0 dhidi ya KMC, mzunguko wa pili, iliyochezwa, Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza, dhidi ya Ihefu, iliyochezwa, Februari 11 akichangia ushindi wa mabao 5-0, na dhidi ya Namungo, iliyochezwa, Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa, Lindi, akifunga bao moja, akichangia ushindi wa mabao 3-1.




## African Sports yabeba 'ndoo' Championship, Kiluvya yapanda

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA wa Ligi ya Jamhuri ya Muungano mwaka 1988, African Sports, imefanikiwa kupanda Ligi ya Championship, na kutwaa ubingwa wa Ligi Daraja la Pili (First League), baada kuifunga Kiluvya FC bao 1-0 katika mechi ya fainali ya ligi hiyo iliyocheza juzi, Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga.

Pamoja na kupoteza mechi hiyo, timu ya Kiluvya FC, nayo imefanikiwa kupanda Ligi ya Championship.

African Sports, na Kiluvya zinakwenda kuchukua nafasi ya Pan African na Ruvu Shooting ambazo zimeshika kutoka Ligi ya Championship, kwenda First League, ambapo ni kama zimebadilishana nafasi.

Timu hiyo ilikabidhiwa kombe lao na Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), Wallace Karia, ambaye alikuwa mgeni rasmi katika mchezo huo.

Kabla ya fainali hiyo, kulikuwa na mechi ya kusaka mshindi wa tatu, ambapo Malimao FC ya Katavi ilimaliza ligi hiyo kwa hasira, baada ya kutoa kipigo cha mabao 7-0 dhidi ya Mwadui, katika mchezo uliochezwa saa 7:00 mchana, kabla ya fainali.

Mabingwa hao wa Tanzania mwaka 1988, walimaliza nafasi ya pili kwenye Kundi A wakiwa na pointi tano, mechi za hatua ya nane bora za First League, na kulazimika kucheza na mshindi wa kwanza wa Kundi B, Mwadui, aliyemaliza na pointi saba, huku Kiluvya ambayo nayo ilishika nafasi ya pili kwenye kundi B, ikiwa na pointi sita, ikifanikiwa kupata nafasi hiyo baada ya kuishinda Malimao FC iliyoongoza Kundi A, ikiwa na pointi sita.

# *Vita ya ubingwa Ligi Kuu Zanzibar yazidi kunoga*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

VITA ya ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar imeendelea kupamba moto kwa timu nne za juu katika msimamo wa ligi hiyo ambayo inadhaminiwa na Benki ya Watu wa Zanzibar PBZ.

Licha ya ligi hiyo kubaki michezo michache kukamilisha msimu huu wa 2023/24, mpaka sasa hakuna timu ambayo inaweza kutabiriwa kuwa bingwa kutokana na kutofautiana pointi kwa alama ndogo kwa timu zilizopo nafasi hizo nne za juu.

Maafande wa JKU SC ndio vinara wa ligi hiyo wakiwa na alama 50, wakati nafasi ya pili ikikaliwa na Zimamoto SC wenye pointi 46, nafasi ya tatu ikishikiliwa na Bingwa Mtetezi, KMKM SC yenye alama 45, huku nafasi ya nne ikikaliwa na KVZ FC yenye pointi 44.

Timu zote tayari zimecheza michezo 23 huku zikibakisha michezo saba kabla ya kutamatika kwa ligi hiyo kwa msimu huu wa 2023-2024.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Zimamoto, Mohmed Hilali, ambae juzi aliiongoza timu yake kupata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Kundemba FC, alisema bado ligi imezidi kuwa ngumu.

Alisema katika hatu hii iliyofikia michezo yote imekuwa migumu bila kuangalia nafasi ya timu iliyopo chini au juu, tofauti na msimu iliyopita.

Alisema kutojulikana mapema kwa timu bingwa na hata kwa baadhi ya zile zinazoshuka daraja hilo limesababisha michezo ya mwishoni kuzidi kuwa migumu.

"Licha ya ugumu wa ligi, lakini bado tupo katika mbio hizi za ubingwa, tutaendelea kupambana kwa kufanya mapitio ya kila mchezo wetu ambao tunacheza ili kuhakikisha makosa hayajirudii katika safari yetu ya kuusaka ubingwa msimu huu," alisema.

Hata hivyo, alisema kufanya vizuri katika michezo mitatu mfululizo kumetokana na hamasa kubwa iliyooneshwa na mashabiki wao, lakini pia wachezaji wenyewe kuwa na hamu kubwa ya kutwaa ubingwa msimu huu.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### RICHARLISON AWANIA SAUDIA

MABINGWA wa Saudi Pro League Al-Hilal, wana uhakika wa kumsajili mshambuliaji wa Tottenham na Brazil, Richarlison, msimu huu, huku Spurs wakiwa tayari kutoa ofa kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27. ***(Mirror)***

### EBERECHI KUBADILISHWA

KLABU ya Totenham Hotspur, inaweza kumbadilisha Richarlison kwa Eberechi Eze wa Crystal Palace mwenye umri wa miaka 25, lakini wanakabiliwa na ushindani kutoka Manchester City kwa winga huyo wa England. ***(Football Insider)***

### RADU ALENGWA NAPOLI

KLABU ya Npoli inamlenga mlinzi wa Tottenham Hotspur na Romania, Radu Dragusin, ambaye alihamia England mnamo Januari, lakini Spurs wanataka pauni milioni 40 kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22. ***(Sun)***

### MASON AGOMBEWA

BARCELONA na Atletico Madrid wanamlenga mshambuliaji wa Uingereza Mason Greenwood mwenye umri wa miaka 22, huku Manchester United wakiweka dau la pauni milioni 51.7 kwa fowadi huyo. ***(Marca)***

### JONG ATAKIWA TENA

KLABU ya Mnchester United itafufua uhamisho wa kiungo wa Barcelona, Frenkie de Jong, 26, baada ya kushindwa kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi mwaka 2022. ***(Mundo Deportivo)***

### MCCLAREN KUBAKI

KOCHA Msaidizi, Steve McClaren, anaweza kubaki Manchester United msimu ujao - hata kama Erik ten Hag na wafanyakazi wengine watafutwa kazi. ***(Mirror)***

### SABA KUUZWA ARSENAL

KLABU ya Arsenal imeweka wazi kuuza wachezaji saba wa kikosi cha kwanza, wakiwamo watatu wa Kimataifa wa Uingereza - kipa Aaron Ramsdale, 25, fowadi Eddie Nketiah (24), na kiungo Emile Smith Rowe, 23. ***(Mirror).***

### ZUBIMENDI HAUZWI

MATUMAINI ya Arsenal kumsajili kiungo wa kati, Martin Zubimendi, 25, yamefifia baada ya Mkufunzi wa Real Sociedad, Imanol Alguacil, kusema kuwa mchezaji huyo hatauzwa msimu huu wa majira ya joto. ***(Metro)***

### GROSS KUONDOKA

KIUNGO wa kati wa Ujerumani, Pascal Gross, 32, anaweza kuondoka Brighton na kujiunga na Eintracht Frankfurt msimu huu wa majira ya joto. ***(Florian Plettenberg)***

### IHEANACHO AWINDWA

KLABU ya Everton ina nia ya kumsajili fowadi wa Leicester City na Nigeria Kelechi Iheanacho mwenye umri wa miaka 27. ***(Football Insider)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI AKERWA SHERIA MPYA SOKA MAREKANI

**MIAMIA,** Marekani

**Ni ile ya majeruhi kutoka nje na kupumzika kwa dakika mbili kabla ya...**

NYOTA wa Inter Miami, Lionel Messi alionesha hasira yake juu ya sheria mpya ya Ligi Kuu ya Soka ya Marekani inayomlazimu mchezaji aliyejeruhiwa kukaa nje ya uwanja kwa dakika mbili, akisema, "Kanuni za aina hii ni mbaya," baada ya kutoka nje ya uwanja wakati wa ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya mwenyeji Montreal Jumamosi usiku.

**Katika dakika ya 40 ya mechi, mlinzi wa Montreal, George Campbell, alimfanyia madhambi fowadi huyo wa Argentina.**

Madaktari wa Miami walikimbilia eneo la tukio kumhudumia mchezaji huyo, lakini Campbell hakuoneshwa kadi ya njano kwa tukio hilo.

Kwa sababu ya kanuni mpya za MLS, mwamuzi hatasimamisha mpira kwa sababu ya jeraha la mchezaji ambaye atabaki uwanjani kwa zaidi ya sekunde 15 na madaktari kuingia uwanjani, mchezaji huyo anaweza kutakiwa kuondoka uwanjani kwa kwa dakika mbili."

Messi alitoka nje ya uwanja katika wakati muhimu, baada ya faulo hiyo kuamsha mpira wa adhabu kwa Miami katika nafasi nzuri kwa mchezaji huyo kufunga.

Katika kipindi kifupi cha kukaa pembeni, mchezaji huyo aligeukia kamera kuonesha dharau huku akitikisa kichwa kwa hasira.

Kutokana na mchezo huo, Kocha wa Miami, Gerardo Martino, alionesha kufadhaika kwa timu juu ya sheria hiyo mpya kwa kuongeza: "Kuna hali ambazo lazima zirekebishwe.

"Katika hali ya Leo, ni wazi alichezewa vibaya. Mchezaji huyo alistahili kadi ya njano, ambayo itamaanisha kuwa Messi hangeweza kuondoka uwanjani kwa dakika mbili. Ninavyoelewa, timu iliyopata faulo iliadhibiwa. Kwa sheria hii mpya mabadiliko, kuna hali ambazo lazima zirekebishwe. Ukiukaji huo ulikuwa wazi na ilikuwa kadi ya njano, na hatimaye ni sisi tuliompoteza Leo kwa dakika mbili."

## HABARI MICHEZO

# ENRIQUE: PSG ITAKUWA BORA ZAIDI KUONDOKA MBAPPE




**PARIS,** Ufaransa

KOCHA Luis Enrique amesisitiza kuwa Paris Saint-Germain itakuwa timu yenye nguvu zaidi msimu ujao licha ya kumpoteza Kylian Mbappe kwa uhamisho wa bure.

Baada ya miezi kadhaa ya uvumi, siri mbaya zaidi ya soka ilifichuliwa Ijumaa jioni Mbappe alipothibitisha kuwa ataondoka PSG baada ya kumalizika kwa mkataba wake msimu huu wa majira ya joto.

Ingawa kumpoteza Mbappe kwa uhamisho wa bure kutaonekana kuwa pigo kubwa la kifedha, PSG wamejilinda kwa muda mrefu kwa makubaliano ya kisheria na Mfaransa huyo ambayo yatawawezesha kurejesha bonasi kubwa ya uaminifu aliyolipwa, na mshahara wake mkubwa pia haupo kwenye vitabu. Na PSG inakadiriwa kuokoa karibu euro milioni 225.

PSG wamejiandaa kuwekeza kiasi kikubwa cha fedha hizo kwenye kikosi cha wachezaji wanaocheza msimu huu wa majira ya joto na Enrique anatarajia kuwa timu hiyo ya Ufaransa itakuwa na nguvu zaidi msimu mpya unapofika.

"Nina uhakika kwamba, bila kujali wachezaji waliopo hapa, nina imani msimu ujao tutakuwa na nguvu zaidi, ndivyo ninavyoona mambo," alisisitiza.

"Licha ya ukweli kwamba mara nyingi watu walitaka kutukabili, na ukweli kwamba Kylian alikanusha mambo, ninachoweza kusema ni kwamba yeye ni mwanasoka mzuri na mtu wa ajabu.

"Ninaelewa uamuzi wake, alikaa miaka saba hapa, alitoa kila kitu kwa ajili ya klabu, na klabu ilimpa kila kitu. "Simlalamikii Kylian kwa kiwango chochote, imekuwa hivyo, yeye ni kiongozi. PSG itaendelea kuwa timu kubwa. Tunataka kusajili wachezaji wenye njaa, wanaotaka kujitambulisha na klabu, lakini mimi ninajivunia kuwa na uzoefu msimu huu na Kylian Mbappe."

Mbappe anatarajiwa kusajiliwa na Real Madrid msimu huu wa majira ya joto, akiongoza safu ya ushambuliaji ambayo tayari ina Vinicius Junior, Rodrygo, Jude Bellingham na Endrick.

"Kylian ni mwanasoka mzuri, mtu wa karibu na wewe, mwenye matumaini, ambaye huwa na tabasamu," Enrique alisema.

# *Kroos, Modric kupewa mikataba*

**MADRID,** Hispania

RAIS wa Real Madrid, Florentino Perez, amepanga kufanya mazungumzo na Toni Kroos na Luka Modric ili kuamua juu ya mustakabali wao katika wiki zijazo, ripoti imedai.

Mkataba wa Kroos na Modric unamalizika msimu huu wa majira ya joto na wanaweza kuondoka Madrid bila malipo mwishoni mwa Juni.

Wawili hao wamekuwa kwenye mikataba ya mwaka mmoja kila mmoja na ingawa walikubali kuongezewa Mei mwaka jana, Marca limeandika kuwa kuna uwezekano mkubwa wa kuamua juu ya kuhama kwao hadi karibu na kumalizika kwa mikataba yao ya sasa.

Madrid wamekuwa wakipanga kikosi chao kwa ajili ya msimu wa 2024/25 tangu Machi na wanatathmini soko ili kuamua kama watoe mikataba mipya kwa Kroos na Modric.

Kocha Carlo Ancelotti angependelea kuwabakiza kwa ajili ya mwendelezo, wakati viwango vyao vimethibitisha kuwa bado wana uwezo wa kucheza.

Madrid haijatoa mapendekezo yoyote makubwa kwa mchezaji yeyote katika miezi ya hivi karibuni na hivyo Perez hivi karibuni atakutana na viungo hao wawili ili kukamilisha mipango.

Kroos na Modric sio wachezaji pekee wa Madrid ambao mikataba yao inamalizika, Lucas Vazquez na nahodha wa klabu Nacho Fernandez pia mikataba yao inakaribia mwisho wa msimu huu.

Ingawa Vazquez anatarajiwa kusaini mkataba mpya na 'Los Blancos', Nacho ataondoka kutafuta changamoto mpya.

Amekuwa akihusishwa na klabu mbalimbali barani Ulaya, wakiwamo mabingwa wa Italia Inter.





# Tuchel hajaamua rasmi pakwenda

**MUNICH,** Ujerumani

THOMAS Tuchel bado hajafanya uamuzi kuhusu mustakabali wake, kwa mujibu wa ESPN.

Ripoti zinadai Tuchel anahisi kama "ana biashara ambayo haijakamilika" katika Ligi Kuu England na anaweza kujaribiwa kurejea, endapo kutakuwa na kazi yoyote inayofaa kwake, lakini bado haijaonekana.

Kocha wa Chelsea, Mauricio Pochettino, ametoa msururu wa majibu yanayozidi kuwa magumu kwa maswali kuhusu hatma yake Stamford Bridge, ambayo yataamuliwa msimu huu wa majira ya joto kutokana na mkutano na wamiliki wa klabu hiyo.

Akiwa United, Erik ten Hag anajikuta kwenye shinikizo kubwa baada ya msururu wa matokeo duni, lakini amesisitiza hadharani kuwa bado ana imani kuwa atasimamia msimu ujao.

Na sasa Tuchel amebainisha kwamba, hajaamua kuhusu mustakabali wake atakapoondoka pale Bayern.

"Sina cha kusema kwa sasa, hakuna sehemu nitakwenda kwa uhakika," alisema Tuchel.



## Simba yaruhusu Yanga kutangaza ubingwa leo

INATOKA UKURASA 24

wa zamani wa timu hiyo, ambaye sasa anaichezea Kagera Sugar, Mbaraka Yusuph.

Kama wasingekuwa wabinafsi, wachezaji Chasambi na Balua wangeweza kuifanya timu hiyo kumaliza dakika 45 na mabao matatu, kwani walipata mpira na kuwalamba chenga mabeki wa timu pinzani, lakini badala ya kutoa pasi kwa wenzao ili wafunge kirahisi, wakalazimisha kufunga wao, badala yake walipiga mashuti yaliyogusa nyavu za pembeni.

Kipindi cha pili, Kagera Sugar walionekana kufunguka, na Simba kukaribisha mashambulizi mengi hadi walipopata bao la kusawazisha.

Baada ya hapo, Kagera Sugar nao walirudi nyuma na kuwaachia wachezaji wa Simba mpira ambao hawakuonekana kuwa wakatili langoni, badala yake walijikuwa wakijichanganya wenyewe.

Moja ya nafasi adhimu walioipata ilikuwa ni dakika kumi kabla ya mechi kumalizika, wakati Balua na Fred walipotegua mtengo wa kuotea na kubaki na kipa Mkongomani, Alain Ngeleka, lakini wao wenyewe waliugombea mpira na kuutoa nje badala ya kuukwamisha wavuni.

## Yanga yanasa mwingine DRC

INATOKA UKURASA 24

wa Yanga, Ali Kamwe, alisema mambo yanaenda vizuri na kila kitu kinasimamiwa ipasavyo na rais wa klabu hiyo, ambapo matumaini makubwa msimu ujao ni kuona Wananchi wakifurahi.

Katika hatua nyingine kikosi cha Yanga leo kinashuka dimbani katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Uwanja wa Manungu Complex uliopo Tuliani, Morogoro.

Kuelekea mchezo huo kocha wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema maandalizi yaneenda vizuri na wanaiheshimu Mtibwa Sugar kwa sababu ipo nyumbani na wapo nafasi ya chini, hivyo itakuwa ikitaka kujinasua kwa kupata matokeo chanya.

"Haitakuwa mechi rahisi kwa sababu wapinzani wanaingia na presha kubwa ya kutaka matokeo chanya, wachezaji wako tayari kwa mchezo huo kwa kupambana kusaka alama tatu," alisema kocha huyo.

Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila alisema wanafahamu ubora wa Yanga na wamejipanga kutafuta pointi muhimu katika mchezo wa leo ili kujinusuru na kushuka daraja.

# WASHINDI 'TWENZETU DUBAI' WAPATIKANA, KUPAA LEO

**Na Mwandishi Wetu**

WASHINDI wawili wa Promosheni ya Twenzetu Dubai na Parimatch inayoendeshwa na Kampuni ya Michezo ya Kubashiri ya Matokeo ya Parimatch wamepatikana na watasafiri leo Jumatatu kwenda Dubai.

Washindi hao ni Daniel Kasanga, mkazi wa Ruvuma na Mohamed Salim mkazi wa Kinondoni, Dar es Salaam, kwa mujibu wa Afisa Uhusiano wa Kampuni ya Parimatch, Ismail Mohamed.

Mohamed amesema Kasanga ni mshindi wa droo ya wiki ya kwanza na Salim ameshinda droo ya wiki ya pili kupitia mchezo Aviator ndani ya Casino.

**Alisema safari hiyo itagharimiwa na kampuni yao ikiwa ni pamoja na usafiri, visa, malazi kwenye hoteli ya kifahari na gharama za kutembelea maeneo mbalimbali ya kitalii na kihistoria wakiwa Dubai.**

"Kasanga na Salim wameshinda tiketi ya Dubai kupitia mchezo wa Aviator ambao unapatikana kwenye Casino ya Parimatch. Bado kuna nafasi za kushinda safari ya kwenda Dubai pamoja na fedha taslim Sh. 200,000 kila siku ambazo zinatolewa katika droo ya siku husika. Tunawaomba wadau wetu kuendelea kubashiri na Parimatch ili kuweza kushinda zawadi hizo," alisema Mohamed.


Kwa upande wa Kasanga alisema amefarijika sana kushinda safari hiyo ya kihistoria kwake.

"Pamoja na kuwa na pasi ya kusafiria, sikujua lini nitaitumia pasi hiyo, hivyo kupitia droo ya Twenzetu Dubai na Parimatch, ndoto yangu imefanikiwa," alisema Kasanga.

Alisema amefarijika kushinda safari hiyo na pia fedha taslimu Sh. 500,000 ambazo alizipata chapchap.

Naye Salim alisema hakuamini mara alipopigiwa simu kuwa ameshinda safari ya Dubai kupitia Promosheni ya Parimatch.

"Sikuamini, kwani unawezaje kwenda kutembelea nchi ya kifahari, yenye raha na vivutio mbalimbali kama Dubai kirahisi rahisi tu. Hata hivyo, kupitia Aviator, jambo hili limewezekana, nawaambia Watanzania wenye umri kuanzia miaka 18, kubashiri




Mkurugenzi Mwendeshaji wa Kampuni ya Parimatch, Eric Gelard (kushoto), akikabidhi tiketi kwa mmoja wa washindi wa Promosheni ya Twenzetu Dubai, Daniel Kasanga, mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NBC yajivunia kuipandisha hadhi Ligi Kuu

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NBC ambayo ni mdhamini Mkuu wa Ligi Kuu Tanzania Bara, imejivunia kuipandisha thamani ligi hiyo tangu ilipoanza kuidhamini miaka mitatu iliyopita ikiwa nafasi ya 12 kwa ubora Barani Afrika mpaka kufikia nafasi ya sita kwa sasa.

Akizungumza kwenye mechi ya Ligi Kuu ya NBC kati ya Azam FC na Simba, iliyopigwa wiki iliyopita katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Mkuu wa Kitengo cha Fedha na Udhamini Benki ya NBC, Joseph Lyuba, alielezea mafanikio makubwa ya ligi hiyo tangu walipoingia kuidhamini miaka mitatu iliyopita.

Lyuba alisema kipindi wakiingia kwenye udhamini huo waliikuta ligi hiyo iko nafasi ya 12 kwa ubora barani Afrika, lakini waliiboresha kwa udhamini wao na kuifanya kufikia nafasi ya sita kwa sasa.

Aliendelea kueleza kwamba kutokana na ubora wa ligi hiyo, sasa hivi imekuwa na mvuto mkubwa hali ilinayosababisha wachezaji na makocha mbalimbali wenye viwango vya juu kutoka mataifa na mabara kufanya kazi nchini.


Aidha meneja huyo aliwaomba wadau wa michezo na watu wengine kuwaunga mkono kwenye kampeni yao ya kuboresha ligi hiyo kwa kutumia huduma za benki hiyo ambazo ni bora na za kisasa zaidi huku zikipatikana nchi nzima.

Nao mashabiki wa soka walizungumza na mwanahabari wetu uwanjani hapo walisifia maendeleo ya ligi hiyo na kukubali kuwa imefanikiwa kwa kiwango cha juu ukilinganisha na miaka kadhaa iliyopita.

"Sisi ni mashabiki wa soka, hivyo kuongezeka kwa ubora wa soka letu hapa nchini ndiyo furaha yetu kama hivi tunawaona makocha wakubwa hapa nchini ambao awali tulikuwa tukiwaona kwenye luninga, lakini sasa hivi tuko nao hapa nchini.

"Hii yote inatokana na ubora wa ligi tuliyonayo, hivyo ni busara kuiunga mkono Benki ya NBC ili ipate morali ya kuendelea kuidhamini na kutuletea uhondo zaidi," alisema shabiki huyo aliyejitambulisha kwa jina Hamdani Juma huku akichanganya utani wa Simba na Yanga.

Michezo
Jumatatu Mei 13, 2024
Nipashe



Tuchel hajaamua rasmi pakwenda UKURASA 22

# Simba yaruhusu Yanga kutangaza ubingwa leo

## ●●● Pia yaipa tena nafasi Azam kuitia mashakani Ligi ya Mabingwa Afrika kwa...

**Na Adam Fungamwango**

BAO lililofungwa na straika wa zamani wa Yanga na Azam, Obrey Chirwa dakika ya 61, limeiweka Simba kwenye mazingira magumu ya kuweza kufuzu Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao, ikilazimishwa sare ya 1-1 dhidi ya Kagera Sugar.

Simba ambayo jana jioni kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera, ilikuwa inamaliza mechi yake ya kiporo, ilitakiwa kushinda ili kuizidi Azam FC kwa kufikisha pointi 59, lakini kwa sare hiyo imetimiza pointi 57 sawa na Wanalambalamba hao, lakini ikisalia nafasi ya tatu ikizidiwa tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa.

**Matokeo hayo sasa yameirahisishia Yanga kutwaa ubingwa wa Tanzania Bara, kwani iwapo itashinda mechi yake ya leo tu, itatawazwa kuwa mfalme wa soka kwa mara ya tatu mfululizo.**

Yanga ambayo leo iko Uwanja wa Manungo Complex, Turiani mkoani Morogoro, kama ikishinda itafikisha pointi 71 ambazo haziwezi tena kufikiwa na timu yoyote kwenye Ligi Kuu.

Simba na Azam iwapo zitashinda mechi zote nne ambazo kila timu imesaliwa nazo, zitafikisha pointi 69.

Hata hivyo, Simba itabidi ijilaumu yenyewe kwa kukosa mabao mengi ya wazi, wakiongozwa na straika wao, Freddy Michael.

Wachezaji wa timu hiyo waliifanya wenyewe mechi kuwa ngumu, ambapo iliwezekana kuimaliza kipindi cha kwanza tu.

Ulikuwa ni uzembe wa beki, Che Malone Fondoh, ambaye alikuwa akimzungusha Abdallah Seseme pembeni mwa uwanja badala ya kuutoa nje, matokeo yake akajichanganya na kuwa kona, iliyopigwa na David Luhende na kuunganishwa vema nyavuni na Chirwa, bao ambalo limewaweka 'Wekundu wa Msimbazi' hao katika mashaka makubwa.

Mechi ilianza kwa kila timu kuonekana kumsoma mwenzake, huku Michael akipaswa ajilaumu mwenyewe kwa kuikosesha Simba bao la wazi dakika ya pili ya mchezo.

Ulikuwa mpira uliorudishwa bila uangalifu na beki wa Kagera Sugar, ambao ulinaswa na straika huyo raia wa Ivory Coast, kabla ya kumvuta upande wa kushoto kipa, lakini akiwa yeye na lango mguu wake ulishindwa kulenga lango na kupiga vyavu za nje, kiasi cha mashabiki wa timu hiyo kutoamini kilichotokea.

Kona fupi iliyopigwa na Luhende dakika ya 15, ilimkuta Mubarack Hamza ambaye aliuingiza langoni, ukapita mbele ya lango la Simba, lakini wachezaji wa Kagera Sugar walizubaa kuuwahi mpira ukatambaa taratibu na kutoka nje ya upande wa pili wa uwanja.

Ilikuwa ni dakika ya 23 wakati Ladack Chasambi, winga aliyesajiliwa dirisha dogo la usajili Januari mwaka huu, akitokea Mtibwa Sugar, alipoipatia Simba bao la shuti kali la mguu wa kulia, nje kidogo la eneo la hatari.

Bao hilo lilitokana na faulo iliyopigwa na Mohamed Hussein 'Tshabalala', iliyomkuta Babakar Sarr, ambaye aliupiga mpira kichwa kuurudisha nyuma, ndipo ulipokutana na mchezaji huyo akiwa katika sehemu nzuri na kuukwamisha wavuni.

Kipa Ayoub Lakred, alifanya kazi ya ziada alipochupa hewani, akiruka pembeni upande wake wa kushoto na kulidaka kwa ustadi shuti kali lililopigwa na straika

INAENDELEA UKURASA 23



Winga wa Simba, Edwin Balua, akipata upinzani mkali kutoka kwa mlinzi wa Kagera Sugar, wakati akijaribu kumtoka kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba, Kagera jana na kumalizika kwa sare ya bao 1-1. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Yanga yanasa mwingine DRC

**Na Saada Akida**

WAKATI ikikabiliwa na kibarua cha kusaka pointi tatu leo dhidi ya Mtibwa Sugar, kwenye Uwanja wa Manungu Complex, Turiani mkoani Morogoro, Klabu ya Yanga inahusishwa kutaka kuwasajili nyota wawili, kiungo mshambuliaji Agee Basiala kutoka Klabu ya AS Maniema ya DR Congo na kipa wa Tanzania Prisons, Yona Amos kwa ajili ya msimu ujao wa mashindano.

Imeelezwa kuwa tayari uongozi wa timu hiyo upo kwenye mazungumzo na wachezaji hao, na kwamba kwa upande wa Basiala mwenye uwezo wa kucheza namba nane na 10 pia akiweza kutokea pembeni, alifanya mazungumzo na Rais wa Yanga, Hersi Said, alipokuwa nchini DR Congo wiki iliyopita.

Pia Yanga, ipo katika harakati za kuhitaji huduma ya kipa Amos, anayewindwa na Wanajangwani hao kuchukua nafasi ya, Metacha Mnata, ambaye tetesi zinaeleza atapewa mkono wa kwa heri mwishoni mwa msimu.

Taarifa za uhakika zilizolifikia Nipashe jana, kutoka ndani ya Yanga, Hersi amefanya mazungumzo na kipa huyo ili kuiongezea nguvu timu yao sambamba na kiungo wa kati Yusuph Kagoma aliyekuwa Singida Fountain Gate FC.

"Mkakati mwingine wa mpango wa klabu unahusisha kipa wa Tanzania Prisons, Yona Amos ni chaguo la kwanza kwa sasa, Yanga inalenga kupata huduma yake ili kuimarisha safu yao ya ulinzi na kuzidi kuimarika kama kikosi kikali katika soka la Tanzania," alisema mtoa habari huyo ndani ya Yanga.

Aliongeza kuwa mazungumzo na kipa huyo bado yanaendelea, na kwamba Yanga imeendelea kujikita katika kudumisha hadhi yake ya kutawala soka la Tanzania, macho yakiwa yanalenga kuendelea kufanikiwa ndani na kimataifa.

Kwa mujibu wa Ofisa Habari

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >